# Kiswahili

## KITABU CHA MWANAFUNZI

### Darasa la Nne



Taasisi ya Elimu Tanzania

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Kiswahili

## Kitabu cha Mwanafunzi
## Darasa la Nne

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 20

Jina la Chapisho: Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978 - 9976 - 61 - 725 - 2

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 08 Mwezi Machi Mwaka 20 18 kuwa kitabu cha Kiada kwa ajili ya Darasa la Nne katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa mwaka 2015

Dkt. Edicome Cornel Shirima
Kaimu Kamishna wa Elimu

## Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la Kwanza 2018
Chapa ya Pili 2021

ISBN: 978-9976-61-725-2

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam - Tanzania

Simu: +255 735 041 170 /+255 735 041 168
Barua pepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

FOR ONLINE USE ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 2 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

Ukurasa

**Utangulizi** ........................................................................ **v**

**Shukurani** ........................................................................ **vi**

**Sura ya Kwanza**
Kutaja neno moja linalobeba maana ya jumla ........................1

**Sura ya Pili**
Vitendawili, nahau na methali ............................................11

**Sura ya Tatu**
Kutambua rangi za vitu ................................................... 21

**Sura ya Nne**
Kueleza matukio ..............................................................26

**Sura ya Tano**
Mavazi yetu ......................................................................36

**Sura ya Sita**
Vinywaji vyetu .................................................................. 45

**Sura ya Saba**
Mimea yetu ...................................................................... 53

**Sura ya Nane**
Zahanati yetu .................................................................... 61

**Sura ya Tisa**
Kazi zinazofanyika kila siku ............................................. 71

**Sura ya Kumi**
Kutumia alama za uandishi .............................................. 80

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya Kumi na Moja**
Kuandika hadithi ........................................................... 86

**Sura ya Kumi na Mbili**
Mahali tulipo ................................................................ 93

**Sura ya Kumi na Tatu**
Dawa za kulevya ........................................................... 98

**Sura ya Kumi na Nne**
Kuchemsha chai ........................................................... 105

**Sura ya Kumi na Tano**
Kuandika barua ............................................................ 112

**Sura ya Kumi na Sita**
Kuandika hadithi fupi kwa kutumia majina ya ndege ..........118

**Sura ya Kumi na Saba**
Kujifunza mashairi ........................................................127

**Sura ya Kumi na Nane**
Haki ya elimu kwa mtoto ...............................................135

**Sura ya Kumi na Tisa**
Kufuata maelekezo ya uelekeo wa pande kuu nne za dunia ....141

**Sura ya Ishirini**
Kusoma ngonjera kwa sauti ...........................................149

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 4 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki kitakuza uwezo wako wa kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika. Pia, kitakuwezesha kutumia msamiati wa lugha ya Kiswahili kwa namna mbalimbali. Kitakujengea uwezo wa kupanga mawazo yako kwa mpangilio na mtiririko unaotakiwa.

Kitabu kina hadithi, habari, mashairi, ngonjera, nyimbo na majigambo. Vyote hivyo vitakuwezesha kujifunza kwa furaha. Pia, kina maswali ya kupima ufahamu wako kutokana na ulichokisikiliza au kukisoma. Vilevile, kina mazoezi mbalimbali yatakayokuwezesha kujenga ujuzi wa somo la Kiswahili.

Soma kwa makini kitabu hiki ili uweze kujenga ujuzi wa kumudu somo la Kiswahili.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 5 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki wakiwemo wachapaji, wasanifu, wahariri, wachoraji na wapiga chapa. Pia, inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa maudhui ya kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Shirika la "Global Partnership for Education (GPE)" kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao "Literacy and Numeracy Education Support (LANES)" kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kutayarisha na kuchapisha kitabu hiki.

Mwisho, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa karibu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.

**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 6 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Kutaja neno moja linalobeba maana ya jumla

Katika sura hii utasoma habari kuhusu mahafali ya Darasa la Saba. Kutokana na habari hiyo utaweza kujifunza kuhusu maneno yenye maana za jumla. Pia, utajifunza maneno ya kundi moja na kuweza kuyatumia katika sentensi.

**Fikiri**

1. Je, umewahi kuhudhuria au kusimuliwa kuhusu mahafali?
2. Unafikiri mahafali ni nini?
3. Mambo gani yalifanyika katika mahafali hayo?
4. Wasimulie wenzako kuhusu mahafali hayo kwa kifupi.

## Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Mahafali ya Darasa la Saba

Leo ni siku ya mahafali ya dada yangu Tunu. Amehitimu Darasa la Saba katika Shule ya Msingi Mtibwa. Jana mwalimu alitutangazia tuwahi shuleni kufanya usafi kabla wageni hawajafika.

Tulifika shuleni saa 12:30 asubuhi na tuligawana kazi kwa madarasa. Wanafunzi wa Darasa la Kwanza na la Pili waliokota takataka eneo lote la shule. Wanafunzi wa Darasa la Tatu na la Nne tulifagia madarasa na kupiga deki. Wanafunzi wa Darasa la Tano na la Sita walikusanya kuni na kuchota maji. Wanafunzi wa Darasa la Saba hawakupangiwa kazi.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 1 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Wapishi waliandaa vyakula mbalimbali kwa ajili ya mahafali. Walipika pilau, wali, ndizi, nyama, njegere na maharage. Pia, walipika mboga za majani ambazo ni mchicha, kisamvu na majani ya kunde. Vilevile, waliandaa matunda kama mananasi, maembe na machungwa.

Jukwaa kubwa liliandaliwa kwa ajili ya wageni watakaokaa katika meza kuu. Pembeni mwa jukwaa hilo, kulikuwa na maturubai yaliyofungwa kwa ajili ya kivuli. Sehemu hiyo ilikuwa ni maalumu kwa wazazi na wageni waalikwa. Maeneo yote ya shule yalipambwa kwa maputo ya rangi ya bluu, kijani na nyekundu.

Ilipofika saa 3:00 asubuhi wazazi na wageni waalikwa walianza kuwasili. Tuliwakaribisha na kuwapeleka sehemu iliyoandaliwa kwa ajili yao. Wahitimu nao walikuwa tayari wameketi sehemu yao wakiwa wamevaa sare za shule.



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 2 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Baada ya nusu saa Mgeni Rasmi aliwasili. Mwenyekiti wa kamati ya shule, mwalimu mkuu na wajumbe wa kamati ya shule walimpokea Mgeni Rasmi. Waliongozana naye hadi meza kuu. Wakati huo wote sisi sote tulisimama, tukipiga makofi, nderemo na vifijo vilisikika huku tukiimba wimbo ufuatao:

*Karibuni wageni wetu, karibuni wageni x 2*
*Karibuni shule ya Mtibwa, karibuni wageni x2*
*Sisi ni nani jama, sisi wanafunzi x2*
*Taifa linatutegemea, wazazi wanatutegemea,*
*Sisi wanafunzi.*

Tuliimba wimbo huo hadi wageni walipokaa kwenye viti. **Mshereheshaji** alimkaribisha Mwalimu Mkuu kwa ajili ya kuwakaribisha na kuwatambulisha wageni. Baada ya utambulisho, vikundi mbalimbali vya burudani **vilitumbuiza**. Kulikuwa na nyimbo, maigizo, mashairi na ngonjera. Wageni waalikwa pamoja na wahitimu walifurahi sana.

Ilipofika saa 6:30 **adhuhuri**, Mgeni Rasmi alipewa nafasi ya kutoa nasaha kwa wahitimu. Aliwatahadharisha kuepukana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Baada ya hapo alitoa zawadi. Zawadi zilitolewa kwa wahitimu waliofanya vizuri katika masomo, nidhamu, uongozi na michezo. Hatimaye aliwakabidhi wahitimu vyeti kisha akapiga picha pamoja nao.

Ilipofika saa 7:30 mchana, wageni pamoja na wahitimu walikwenda kupata chakula. Wanafunzi wengine tulikwenda kupata chakula katika madarasa yetu. Ilipofika saa 9:30 **alasiri** wageni waliondoka na wanafunzi tuliruhusiwa kurudi nyumbani.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Katika shule ya Mtibwa kulikuwa na tukio gani?
2. Kazi gani walizifanya wanafunzi shuleni?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Kwa nini wanafunzi wa Darasa la Saba hawakupangiwa kazi?
4. Wapishi walipika nini?
5. Mgeni Rasmi aliwaasa nini wahitimu?
6. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?
7. Je, unajifunza nini kutokana na picha iliyomo katika habari hii?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. mahafali
2. alfajiri
3. wasili
4. alasiri
5. adhuhuri
6. hitimu
7. mshereheshaji
8. kutumbuiza

## Zoezi la 3 Mazoezi ya lugha

**A. Kamilisha jedwali lifuatalo kutokana na habari uliyoisoma kwa kuonesha muda na tukio.**

| Namba | Muda | Tukio |
|---|---|---|
| i. | 12:30 asubuhi | Wanafunzi kufanya usafi katika maeneo ya shule. |
| ii. | 3:00 asubuhi | |
| iii. | | Mgeni rasmi kuwasili shuleni. |
| iv. | | Mgeni rasmi kutoa nasaha. |
| v. | 7:30 mchana | |
| vi. | | Wageni kuondoka na wanafunzi kuruhusiwa kurudi nyumbani. |



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 4 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Andika maneno manne (4) yanayowakilishwa na neno la jumla. Namba moja (i) ni mfano.**

| Namba | Neno la jumla | Maneno |
|---|---|---|
| i. | nguo | *sketi, kaptura, shati, fulana* |
| ii. | rangi | |
| iii. | mboga/kitoweo | |
| iv. | wanyama/viumbe hai | |
| v. | vinywaji | |
| vi. | michezo | |
| vii. | matunda | |
| viii. | mikoa | |
| ix. | wadudu | |
| x. | vyakula | |

**C. Pigia mstari neno lililo tofauti na maneno mengine katika kundi.**

***Mfano:*** *kanga, mwewe, kalamu, njiwa .*

1. sufuria, bakuli, kikombe, viatu.
2. nyumba, gari, pikipiki, baiskeli.
3. shati, suruali, taa, gauni.
4. Ali, Juma, kunguru, Maria.
5. macho, pua, mboga, mdomo.
6. karoti, hoho, vitunguu, chupa.
7. baba, mama, ndama, mjomba.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 5 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D.** **Unda maneno ya jumla kwa kutumia herufi na namba zilizomo katika jedwali hapa chini.**

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | B | CH | D | E | F | G | H | I | J | K | L | M | N | O | P | R |

| 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | T | U | V | W | Y | Z |

***Mfano:***

| 22 | 1 | 14 | 23 | 1 | 13 | 1 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| W | A | N | Y | A | M | A |

**1.**

| 13 | 9 | 13 | 5 | 1 |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

**2.**

| 13 | 9 | 19 | 9 |
|---|---|---|---|
| | | | |

**3.**

| 21 | 23 | 15 | 13 | 2 | 15 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

**4.**

| 22 | 1 | 4 | 20 | 4 | 20 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

**5.**

| 14 | 4 | 5 | 7 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 6 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## E. (i) Cheza na wenzako mchezo ufuatao:

Simameni katika umbo la duara huku mkiwa mmeshikana mikono. Kisha kiongozi ataje maneno yaliyokolezwa rangi na ninyi mtajibu alichokisema kiongozi. Kiongozi atataja majina ya vitu mbalimbali vilivyokolezwa rangi. Endapo kilichosemwa ni sahihi mruke na kuitikia kwa kutaja jina la jumla la kitu alichokitaja. Kama si sahihi msiruke, mkae kimya. Atakayekosea atoke nje ya mduara. Mmoja atakayebaki mpaka mwisho ndiye mshindi.



**Mnyama mnyama mnyama** – mnyama

**Ng'ombe** – mnyama
**Mbuzi** – mnyama
**Gari** – *(kimya)*
**Kondoo** – mnyama

**Tunda tunda tunda** – tunda

**Nanasi** – tunda
**Kijiko** – *(kimya)*
**Parachichi** – tunda
**Chungwa** – tunda

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mti mti mti** – mti

**Mfenesi** – mti
**Waridi** – (*kimya*)
**Mchungwa** – mti
**Mchongoma** – mti

**Ndege ndege ndege** – ndege

**Kuku** – ndege
**Bata** – ndege
**Popo** – (*kimya*)
**Kasuku** – ndege

**Samaki samaki samaki** – samaki

**Sato** – samaki
**Kambare** – samaki
**Nyoka** – (*kimya*)
**Kibua** – samaki

**(ii) Taja majina ya jumla yaliyotajwa katika mchezo uliocheza.**

## Zoezi la 4 Utungaji

**A. Simulia sherehe uliyowahi kuhudhuria.**

**B. Andika habari uliyoisimulia kwa kuzingatia mwongozo ufuatao.**

1. Kichwa cha habari.
2. Nani walishiriki katika sherehe hiyo?
3. Kitu gani kilifanyika kabla ya sherehe?
4. Mambo gani yalifanyika wakati wa sherehe?
5. Kitu gani kilikufurahisha katika sherehe hiyo?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 8 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ufahamu

### Soma na wenzako kisha muigize majigambo yafuatayo:

**Tunda:** Mimi ni tunda, tukiwa wengi tunaitwa matunda. Matunda hayo yanaweza kuwa maembe, ndizi, mananasi au mapapai. Kazi yetu ni kuwapatia binadamu vitamini. Binadamu akitumia matunda atajikinga na maradhi. Pia, ataongeza damu mwilini. Nani kama tunda?

**Mti:** Mimi ni mti, tukiwa wengi tunaitwa miti. Kuna miti ya miembe, michungwa, mipera au miarobaini. Miti ina faida nyingi sana. Miti huzuia mmomonyoko wa udongo. Baadhi ya miti hutoa matunda. Majani, mizizi pamoja na magome ya miti hutumiwa na binadamu kutengeneza dawa. Miti hutoa hewa ya oksijeni na huleta mvua. Nani kama mti?

**Mnyama:** Mimi ni mnyama, tukiwa wengi tunaitwa wanyama. Kuna ng'ombe, mbuzi au kondoo. Huwapatia binadamu kitoweo, mbolea pamoja na maziwa. Ngozi yangu hutumika kutengenezea mikoba, viatu pamoja na mikanda. Nyama yangu husafirishwa nje ya nchi, hivyo husaidia kuinua uchumi wa nchi. Nani kama mnyama?

**Mdudu:** Mimi ni mdudu, tukiwa wengi tunaitwa wadudu. Tunaweza kuwa nyuki, nzi, mbu, panzi, siafu, mende, nge au buibui. Miongoni mwetu wengine ni hatari na wengine si hatari. Tunamsaidia binadamu kupata majibu ya vitendawili vyake. Kama huamini tegua vitendawili vifuatavyo:

1. Ana miguu ya msumeno..................
2. Anang'ata kwa mkia.........................

Nani kama mdudu?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 9 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5 Ufahamu

1. Katika majigambo uliyosoma, kati ya tunda, mti, mnyama na mdudu unapenda kuwa nani? Kwa nini?
2. Eleza faida nyingine za miti ambazo hazikutajwa katika majigambo uliyosoma.
3. Katika majigambo uliyosoma mdudu anasema, "Miongoni mwetu wengine ni hatari na wengine si hatari." Taja wadudu ambao ni hatari na wasio hatari kwa binadamu.

## Zoezi la 6 Zoezi la lugha

**Kanusha sentensi zifuatazo:**

***Mfano:*** *Watoto wanacheza ngoma.*
*Watoto hawachezi ngoma.*

1. Sisi tunakula nyama ya ng'ombe.
2. Mama hupika chakula na mboga za majani.
3. Sufuria, bakuli na vijiko hupatikana darasani.
4. Samaki ni chakula chenye wanga.
5. Mbwa anakula majani.
6. Popo hutaga mayai.

## Zoezi la 7 Utungaji

**Andika majigambo kwa kutumia vyombo viwili vya usafiri.**

*Mfano: Baiskeli:* Mimi ni baiskeli.
Ni usafiri rahisi na wenye gharama nafuu.

Kila mtu anaweza kuninunua. Nani kama baiskeli?



FOR ONLINE USE ONLY

Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 10 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Vitendawili, nahau na methali

Katika sura hii utajifunza namna ya kutega na kutegua vitendawili. Pia, kueleza maana ya nahau. Kisha, utaweza kukamilisha methali, kuelezea maana zake na kufafanua ujumbe uliomo. Vilevile, utaweza kueleza umuhimu wa vitendawili, nahau na methali.

**Fikiri**

Chunguza kila sentensi kisha taja sentensi hiyo ni kitendawili au methali?

1. Polepole, ndio mwendo.
2. Athumani mfupi kasimama mlangoni.
3. Jogoo wa shamba, hawiki mjini.
4. Kila mtu humwabudu apitapo.

## Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Doto mshindi

Siku ya Jumamosi ni siku ya mapumziko. Mimi na wadogo zangu Ngwila na Aisha hatuendi shule. Tunafua nguo zetu za nyumbani na sare za shule. Pia tunawasaidia wazazi kazi za nyumbani.
Siku hiyo nilitembelewa na marafiki zangu Kulwa na Doto. Walipofika nyumbani kwetu walifurahia mazingira ya nyumba yetu.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 11 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Doto alisema, “Rafiki yangu Tumaini, nyumba yenu ni safi na inapendeza sana. Maua yamepandwa kwa mpangilio mzuri.” Kulwa naye aliongeza, “Rangi mbalimbali zilizopakwa zinaifanya nyumba yenu ipendeze zaidi.” Niliwaeleza kuwa siku za mapumziko tunawasaidia wazazi wetu kufanya usafi wa mazingira. Vilevile, tunamwagilia bustani ya maua. Doto naye alisema, “Kweli ninyi ni mfano bora wa kuigwa. Mazingira safi ni muhimu kwa afya zetu.”

Siku hiyo baba alinunua matunda na mama alitupikia chakula kizuri. Baada ya chakula cha mchana tulikaa barazani na kutega vitendawili. Tulimkaribisha kaka ili aweze kusikiliza jinsi tunavyotega na kutegua vitendawili. Kaka alituambia yeye ataandika alama za kila mmoja wetu. Alitueleza kuwa atakayetega kitendawili na wengine wakashindwa kutegua, atakuwa amepata alama. Hivyo mshindi atakuwa ni yule aliyepata alama nyingi.



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 12 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Mazungumzo yetu katika kutega vitendawili yalikuwa kama ifuatavyo:

**Mimi:** Kitendawili?

**Wote:** Tega.

**Mimi:** Ukoo wetu hauishiwi na safari.

**Kulwa:** Gari.

**Mimi:** Umekosa.

**Aisha:** Pikipiki.

**Mimi:** Umekosa. Nipeni mji.

**Doto:** Nenda Dodoma.

**Mimi:** Sawa naenda Dodoma nikirudi nitawaletea zabibu. Ukoo wetu hauishiwi na safari jibu lake ni siafu.

**Kulwa:** Sasa ni zamu yangu. Kitendawili?

**Wote:** Tega.

**Kulwa:** Ubwabwa wa mwana mtamu.

**Aisha:** Mahindi.

**Kulwa:** Umekosa

**Doto:** Usingizi.

**Kulwa:** Umepata.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tulishindana kutega vitendawili kwa saa moja. Mimi nilitegua kitendawili kimoja. Aisha alitegua vitendawili viwili na Doto aliweza kutegua vitendawili vitatu. Kaka alimtangaza Doto kuwa ndiye mshindi. Wote tulimpigia makofi ya kumshangilia. Kaka alituambia, "Ninyi ni hodari wa kutega vitendawili." Baada ya kuona usiku umeingia, kaka aliwaambia Kulwa na Doto warudi nyumbani. Wote tulisimama na kuwasindikiza rafiki zetu.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Tumaini alikuwa na wadogo zake wangapi?
2. Doto alipofika nyumbani kwa akina Tumaini alifurahia nini?
3. Je, tunapaswa kufanya nini siku za mapumziko?
4. Tumaini, Aisha na rafiki zao walikuwa wakifanya nini barazani?
5. Kwa nini Doto alishinda?

## Zoezi la 2 Vitendawili

**A. Tegua vitendawili vifuatavyo kwa kutumia picha.**

*Mfano: Bibi hatui mzigo wake.* ***Kobe***

(i)

(ii)

(iii)

(iv)

(v)


1. Kiota changu kimezungushiwa boma la nyasi. ________
2. Kila mtu humwabudu apitapo. ____________
3. Kaa hapa nikae pale tumfinye mchawi. ____________
4. Kilemba chake haazimishi. ____________

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 14 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Tegua vitendawili vifuatavyo:**

1. Mjomba hataki tuonane. ___________
2. Watoto wa binamu wakiondoka hawarudi. ___________
3. Mtoto wangu ana mguu mmoja kila mtu anamwabudu. ___________
4. Hana miguu lakini huenda mbio sana. ___________
5. Kila niendapo hunifuata. ___________
6. Kamba yangu ndefu lakini haiwezi kufunga mzigo wa kuni. ___________
7. Bomu la machozi baridi. ___________
8. Nyumba yangu ina mlango juu. ___________

**C. Andika vitendawili vyenye majibu yafuatayo:**

***Mfano:*** *Macho    Popoo mbili zavuka mto.*

1. mhindi ___________
2. mwiba ___________
3. utelezi ___________
4. konokono ___________
5. ngoma ___________

## Zoezi la 3 Zoezi la lugha

**Andika KWELI au SI KWELI.**

1. Watoto hawapaswi kujua vitendawili. __________
2. Vitendawili ni maneno yanayoficha maana ya kitu ili kisijulikane kwa urahisi. __________
3. Katika vitendawili mtu anapopewa mji anaweza kuukubali au kuukataa. ________
4. Vitendawili husaidia kuhusisha vitu vilivyomo katika mazingira yetu. ________
5. Vitendawili havifikirishi. ________

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 15    7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4 Nahau

**Tumia nahau zifuatazo kukamilisha maelezo uliyopewa.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| tia moyo | kufa kishujaa | piga chenga | piga yowe |
| piga mbizi | kata tamaa | piga marufuku | |

***Kwa mfano:***

Sanga ni mkulima wa mahindi. Mafuriko yalipotokea mazao yake yote yalizolewa na maji. Baada ya mwezi mmoja mvua ilikatika. Sanga hakutaka tena kurudia kupanda mahindi. Je, Sanga alifanya nini? Sanga **alikata tamaa**.

**Maelezo:**

1. Mwalimu Chapakazi aliwaambia wanafunzi warudi nyumbani. Wengine walimkwepa na kurudi tena kutazama mafuriko. Wanafunzi hao watakuwa wamemfanyia nini mwalimu wao?
2. Bahati alipokaribia kuzama alijua ndio mwisho wa uhai wake. Maneno aliyoambiwa na wanafunzi wenzake yalimwezesha kuamini kuwa atatoka salama. Je, maneno ya wanafunzi hao yalimfanya nini Bahati?
3. Kama Musa angezama na kupoteza maisha wakati akimuokoa Bahati, angekuwa amefanya nini?
4. Wanafunzi walipomuona Bahati anazama walipiga kelele. Wengine walifanya nini ili kumpa msaada?
5. Mara baada ya kuzolewa na maji Bahati alijiona yuko hatarini. Alifanya nini ili kujiokoa?

## Zoezi la 5 Methali

**A.** *Soma hadithi ifuatayo kisha andika methali zilizomo na maana zake.*

## Umoja ni nguvu

“Ama kweli **kuishi kwingi, ni kuona mengi**.” Nilimsikia bibi



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 16 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

akiongea maneno hayo peke yake. Sikusita kumkaribia na kumuuliza, "Bibi unaongea na nani?" Bibi alijibu, "Nimekumbuka habari ya kijana aitwaye Besao. Ngoja nikusimulie mjukuu wangu."

Besao ni mtoto wa kwanza kuzaliwa katika familia yenye watoto wanne. Besao hakupenda kushirikiana na wadogo zake katika mambo mbalimbali. Alikuwa mbinafsi na alifanya kila kitu peke yake. Aliamini kuwa **wingi si, hoja**. Mama yake alimwambia kuwa, **kidole kimoja, hakivunji chawa**.

Siku moja Besao aliumia mguu. Ndugu zake walishirikiana kumuuguza hadi alipopona. Baada ya kupona mguu Besao aliona aibu sana. Aliwaomba radhi wazazi na wadogo zake.

Besao aliwaambia kwamba ameamini kuwa, **umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu**. Kuanzia hapo Besao alianza kushirikiana na wadogo zake.

### B. Tumia methali zifuatazo kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika maelezo uliyopewa 1 - 4.

**Methali**

(a) Umoja ni nguvu, na utengano ni udhaifu.
(b) Jungu kuu, halikosi ukoko.
(c) Akiba, haiozi.
(d) Kilema si, ugonjwa.

**Maelezo**

1. Baraka ni mlemavu wa mkono. Hufanya kazi kwa bidii kama watu wengine. Baraka hapendi ulemavu umfanye awe mvivu.

   ..........................................................................................

2. Besao ni mtu ambaye hapendi kushirikiana na wenzake. Muda mwingi hupenda kuwa peke yake na mambo yake mengi hayafanikiwi.

   ..........................................................................................

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 17 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Mawazo ni Mwenyekiti wa kijiji. Ni mtu mwema na mwenye busara. Wanakijiji wanapotaka kutatua jambo hupenda kwenda kwake kwa ajili ya ushauri.

.....................................................................................................

4. Familia inatunza mazao waliyovuna kwa ajili ya matumizi wakati wa njaa.

.....................................................................................................

## C. Kamilisha methali zifuatazo:

1. Kuku mgeni, ________________________.
2. Kuvuja kwa pakacha, ________________.
3. Jogoo wa shamba, __________________.
4. Dau la mnyonge,_____________________.
5. Leo ni leo, __________________________.

## D. Andika methali zitakazotumika kuwaonya watu wenye tabia zifuatazo:

***Mfano:***

*Mtu asiyesikiliza ushauri anaopewa na wakubwa zake.*
*Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.*

1. Mtu asiyetaka kushughulikia jambo dogo ambalo mwishowe humletea matatizo makubwa.

   _________________________

2. Mtu anayependa kuchagua sana na kushindwa kufanya uamuzi.

   _________________________

3. Malezi mabaya ya wazazi kwa watoto wao.

   _________________________

4. Mtu ambaye ni mgeni mahali fulani na huonesha tabia

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

zake tofauti na za wenyeji wake.

________________________

5. Mtu anayependa kuuliza maswali sana ili kuelewa jambo.

________________________

6. Mtu anayependa kutunza vitu kwa manufaa ya baadaye.

________________________

7. Mtu aliyeonywa na wazazi wake akashindikana ataonywa na jamii.

________________________

## Zoezi la 6 Mazoezi ya lugha

**A. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wakati ujao.**

1. Bibi aliongea peke yake.
2. Besao aliwaomba radhi ndugu zake.
3. Bibi anatusimulia hadithi.
4. Wanafunzi walirudi shuleni mapema.
5. Wanafunzi wanaandika vizuri sana.
6. Dada anamwagilia bustani ya miti.
7. Wazazi waliwahi kwenye mkutano.
8. Sherehe ya watoto ilianza mapema.

**B. Andika sentensi zifuatazo katika hali timilifu.**

1. Magugu yanaota bondeni.
2. Askari anabeba bunduki.
3. Mwalimu wetu anatufundisha vizuri.
4. Sahani ilivunjika.
5. Mwalimu anafundisha somo la Kiswahili vizuri.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 19 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Maji yanamwagika.
7. Wanafunzi wanaimba wimbo wa taifa.
8. Jua linazama mapema.
9. Mapera yanadondoka.
10. Kaka anatupikia chakula kitamu.

## C. Oanisha methali zinazofanana kutoka sehemu A na B.

***Mfano:*** *1. Kidole kimoja, hakivunji chawa*
*(f) <u>Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.</u>*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| i. Kidole kimoja, hakivunji chawa _f_ | (a) Usipoziba ufa, utajenga ukuta |
| ii. Mdharau mwiba, mguu huota tende…...... | (b) Mchagua nazi, huambulia koroma |
| iii. Mchagua jembe, si mkulima…... | (c) Mchumia juani, hulia kivulini |
| iv. Samaki mkunje, angali mbichi…... | (d) Haraka haraka, haina baraka |
| v. Polepole ndio, mwendo………. | (e) Mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo |
| vi. Jembe halimtupi, mkulima…….. | (f) Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu |

## D. Andika sentensi zifuatazo katika hali ya ukanushi.

1. Kwasi alikuwa hodari katika masomo yake shuleni.
2. Rafiki yangu alipenda sana michezo.
3. Kuku alitaga mayai mengi.
4. Tuliambiwa twende shuleni kumwagilia miti.
5. Juma ni mkarimu sana.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Kutambua rangi za vitu

Katika sura hii utasoma habari kuhusu mwaka mpya. Kutokana na habari hii utaweza kujifunza kutambua rangi za vitu. Vilevile utajifunza kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanyika katika nyakati mbalimbali za siku.

**Fikiri**

Ni shughuli zipi zinazofanyika wakati wa sherehe za mwaka mpya?

### Ufahamu

*Soma habari hii, kisha jibu maswali.*

**Mwaka mpya**

Watoto, vijana na wazee waliandaa michezo ya sherehe za mwaka mpya. Waliandaa ngoma, nyimbo na **sarakasi** kwa ajili ya sherehe hizo. Mwaka huu mdogo wangu Bahati aliingia Darasa la Pili na mimi niliingia Darasa la Nne.

Wiki iliyopita baba na mama walitupeleka kwa bibi yetu kusalimia. Tulisafiri kuanzia asubuhi na tukafika jioni. Bibi alitupokea kwa shangwe. Tulikaa kwa bibi kwa muda wa siku mbili tu.

Baada ya hapo tulianza safari ya kurudi nyumbani. Siku hiyo **mvua za rasharasha** zilikuwa zinanyesha. Tulipumzika siku moja, kisha siku iliyofuata tulikwenda madukani. Mimi nilivaa kaptura nyeusi na fulana nyekundu, baba suruali ya kijani, mama sketi ya zambarau na mdogo wangu gauni jekundu. Tuliondoka nyumbani asubuhi na mapema. Mama alituambia tuwahi kwenda kabla ya jua kuwa kali.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 21 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tulipofika madukani tulikwenda moja kwa moja kwenye duka la viatu na mabegi. Mdogo wangu alinunua begi lenye rangi ya kijivu na zambarau. Mimi nilinunua begi lenye rangi ya kijani.




Ilipofika mchana tulikwenda kula **mgahawani**. Chakula kilikuwa kitamu sana. Baada ya kula tulirudi tena madukani. Tulikwenda moja kwa moja kwa fundi **cherehani**. Tulikuta **sare** zetu tulizopima zimeshonwa na **kupigwa pasi**. Zilikuwa za rangi nyeupe na bluu. Safari yetu haikuishia hapo, tulikwenda duka lililo karibu. Tukanunua viatu vyeusi na soksi nyeupe. Tulirudi nyumbani wakati jua limekaribia kuzama.

Jumatatu ilipofika, mama alituamsha asubuhi na mapema ili tuwahi shuleni. Kama kawaida, **alitutia moyo** na kutuambia tusome kwa bidii ili tufaulu vizuri. Tulijiandaa kisha baba na mama walitusindikiza. Walipenda kuona madarasa yetu na kuwaona walimu wetu wapya. Tulipofika shuleni tulioneshwa bustani za kumwagilia na maeneo ya kufanya usafi. Baada ya hapo, tuliingia darasani na kutambulishwa kwa walimu wetu wapya.

Mimi na mdogo wangu tulikuwa na furaha sana. Tulifurahia kukutana na walimu wapya, madarasa mapya na kuvaa sare mpya.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 22 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Habari hii inahusu nini?
2. Je, watoto waliotajwa katika habari hii waliingia madarasa gani?
3. Nani aliwapeleka kwa bibi yao?
4. Je, walikaa kwa bibi yao siku ngapi?
5. Kwa nini wazazi wao waliwasindikiza shuleni?
6. Fundi cherehani anafanya kazi gani?

.

## Zoezi la 2 Miundo

**Tunga sentensi kwa kutumia miundo ifuatayo:**

***Mfano:*** *Baba alimwambia mama hatuna budi kuwapeleka watoto shuleni.*

1. ……….. kwa ajili ya …………...
2. ………… kwa muda wa ………
3. …………. baada ya …………
4. ……………. ili ……………....
5. …………hatuna budi……...

## Zoezi la 3 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. pasi
2. cherehani
3. sarakasi
4. sare
5. mgahawa

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 23 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4 Nahau

**Eleza maana ya nahau zifuatazo kisha tunga sentensi mbili (2) kwa kila nahau.**

1. piga pasi
2. tia moyo
3. mvua za rasharasha

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A. Andika wingi wa maneno yafuatayo:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| i. mchezo | |
| ii. kifaa | |
| iii. nguo | |
| iv. chakula | |
| v. duka | |
| vi. mvua | |
| vii. bustani | |
| viii. eneo | |
| ix. kiatu | |
| x. begi | |

**B. Andika majina ya vitu viwili kwa kila jina la rangi zifuatazo:**

| | |
|---|---|
| i. nyekundu | |
| ii. njano | |
| iii. zambarau | |
| iv. nyeupe | |
| v. kijivu | |
| vi. nyeusi | |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 24 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika umoja.**

1. Vijana waliandaa michezo mbalimbali.
2. Wazazi watawanunulia watoto wao sare mpya za shule.
3. Wanafunzi wanamwagilia bustani za mboga.
4. Wanafunzi walifanya usafi.
5. Tulikula vyakula migahawani.
6. Tulinunua sare za shule na viatu madukani.

**D. Andika shughuli zinazofanyika katika muda ufuatao:**

1. asubuhi
2. mchana
3. jioni
4. usiku

**E. Andika sentensi zifuatazo katika hali ya ukanushi.**

1. Wakati wa likizo tutakwenda kwa mjomba wetu.
2. Baada ya kula tulirudi tena dukani.
3. Tulisafiri kwa treni kwenda kwa bibi.
4. Kilimo cha bustani ni shughuli ya wakati wa masika.
5. Asubuhi ni wakati wa jua kali.
6. Wanafunzi wanafagia muda wote.

## Zoezi la 6 Utungaji

**Andika habari yenye maneno yasiyopungua sitini (60) ukieleza jinsi ulivyoingia darasa jipya.**

Maswali yafuatayo yatakuongoza.

1. Mwaka uliopita ulikuwa darasa la ngapi?
2. Mwaka huu umeingia darasa la ngapi?
3. Mambo gani umefurahia baada ya kuingia darasa jipya?
4. Unatarajia kufanya nini ili kufanikiwa katika masomo yako?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Kueleza matukio

Katika sura hii utajifunza jinsi ya kueleza matukio mbalimbali kwa usahihi. Utaweza kutumia nyakati mbalimbali kuelezea matukio. Vilevile, utaweza kukanusha matukio katika sentensi kwa kutumia wakati husika.

### Fikiri

Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali:



1. Tukio gani linaonekana katika picha hiyo?
2. Tukio hilo limetokea wapi?
3. Nani walikuwepo katika tukio hilo?
4. Umejifunza nini kutokana na tukio ulililoliona?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 26 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Mafuriko ya mto Zoazoa

Ulikuwa msimu wa masika wenye mvua nyingi na upepo mkali. Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mtakuja walikuwa wanakwenda shuleni. Shule ya Msingi Mtakuja ipo ng'ambo ya Mto Zoazoa. Jina la mto huo lilitokana na tabia ya kuzoa vitu na kuacha huzuni kwa wanakijiji. Pia, ulileta adha kwa wanafunzi ambao hufika shuleni kwa kuuvuka.

Siku moja mto Zoazoa ulifurika. Mazao yaliyopandwa karibu na mto yalisombwa na maji. Baadhi ya nyumba zilibomoka. Watu walioishi karibu na mto huo walipata hasara. Wanafunzi **walipigwa marufuku** kuvuka katika daraja la mto huo ukiwa umefurika. Mwanafunzi mmoja aitwaye Ndekia alikuwa mkaidi. Alidharau kiasi cha maji yaliyokuwa yanapita juu ya daraja na kuamua kuvuka mto. Alipofika katikati ya daraja maji yalimzidi nguvu na kumzoa kuelekea bondeni. Ndekia alijaribu kuogelea ili kujiokoa. Wanafunzi wenzake waliokuwa pembeni walianza kupiga kelele, "Ndekiaa! Ndekiaaa! Shika huo mti unaoelea." Ndekia alishika tawi la mti uliokuwa ukielea. Sauti ya mwanafunzi mwingine aitwaye Huruma ilisikika, "Ndekia, inua kichwa juu..., shikilia vizuri hilo tawi la mti na usikaze mwili wako." Ndekia alifuata maelekezo aliyopewa na Huruma. Wanafunzi wengine walikuwa **wakipiga mayowe** wakiomba msaada.

Mti uliokuwa ukielekea bondeni ulikwama kwenye mbuyu ulioangukia mtoni. Ndekia aliendelea kushikilia tawi la mti. Watu walianza kusogea darajani. Kijana aitwaye Chacha **alijitosa** mtoni kumuokoa. Alipiga makasia na kumuokoa Ndekia. Baada ya kuokolewa Ndekia alilazwa kifudifudi na kuminywa mgongoni ili maji yatoke. Baadaye alipelekwa zahanati.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mwalimu Sara alikuwa zamu shuleni. Aliwatangazia wanafunzi kutokwenda kwenye eneo la mto lililojaa maji. Mwalimu Mbilo na wanafunzi waliokuwa wakiishi ng'ambo ya mto hawakuweza kufika shuleni. Alimpigia simu mwalimu Sara kumweleza yaliyotokea. Mazungumzo yao yalikuwa hivi:

**Mwalimu Mbilo:** Haloo! Haloo! Mwalimu Mbilo anaongea.

**Mwalimu Sara:** Ndiyo mwalimu, habari za asubuhi?

**Mwalimu Mbilo:** Si nzuri. Mto Zoazoa umefurika. Mimi na baadhi ya wanafunzi tumeshindwa kuvuka.

**Mwalimu Sara:** Ni kweli. Tafadhali naomba uwatangazie wanafunzi warudi nyumbani hadi maji yatakapopungua. Naomba uangalie wengine wasije waka**kupiga chenga** na kurudi mtoni.

**Mwalimu Mbilo:** Sawa mwalimu nimekuelewa.

Baada ya mazungumzo hayo, mwalimu Mbilo aliwatangazia wanafunzi wote warudi nyumbani. Aliwaeleza kuwa mafuriko ni ya muda mfupi tu. Maji yatakapopungua wataweza kufika shuleni na kuendelea na masomo.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Habari uliyosoma inahusu tukio gani?
2. Kwa nini mto Zoazoa ulifurika?
3. Ndekia alikuwa na tabia gani?
4. Kwa nini wanafunzi waliokuwa mtoni walipiga kelele?
5. Wanafunzi walifanya nini ili kumsaidia Ndekia?
6. Kingetokea nini kama Ndekia asingesikiliza ushauri wa wenzake?
7. Kwa nini Ndekia aliminywa mgongo baada ya kuokolewa?
8. Kwa nini mwalimu Mbilo aliamua kupiga simu kwa mwalimu Sara?
9. Habari uliyosoma inakufundisha nini?



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 28 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno kwa kutumia wakati uliopo.**

1. masika
2. mkaidi
3. elea
4. adha
5. ng'ambo
6. bondeni
7. kujitosa

## Zoezi la 3 Mazoezi ya lugha

### A. Kazi za kufanya

1. Simulia tukio ulilosoma kwa maneno yako mwenyewe.
2. Igiza na wenzako kuhusu mazungumzo kati ya **mwalimu Sara na mwalimu Mbilo**.

### B. Andika maana ya maneno ya kifungu A kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kifungu B.

**Mfano:** i. adha (c) *jambo linalosumbua au kuleta shida*

| Kifungu A | Kifungu B |
|---|---|
| i. adha | (a) mtu mwenye tabia ya kutosikia anayoambiwa |
| ii. vuli | (b) kipindi cha jua kali |
| iii. ng'ambo | (c) jambo linalosumbua au kuleta shida |
| iv. kiangazi | (d) msimu wa mvua nyingi |
| v. mkaidi | (e) mvua za rasharasha |
| vi. kipupwe | (f) kataza kufanyika au kutumika kwa jambo |
| vii. masika | (g) jaa kupita kiasi |
| viii. furika | (h) upande wa pili wa mto, barabara au bahari |
| | (i) kipindi cha baridi kali |
| | (j) furaha |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Panga sentensi zifuatazo kwa mfuatano sahihi wa matukio.**

1. Siku hiyo mvua kubwa ilikuwa inanyesha.
2. Ilikuwa siku ya Jumatatu.
3. Walipofika katika mto Zoazoa walikuta daraja limefunikwa na maji.
4. Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mtakuja walikuwa wanaelekea shuleni.
5. Mwalimu Mbilo aliwatangazia wanafunzi wote warudi nyumbani.
6. Wanafunzi walishindwa kuvuka mto.

**D. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

1. masika __________
2. zamani __________
3. bondeni __________
4. furaha __________
5. mbali __________
6. faida __________
7. achia __________
8. toka __________

**E. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi:**

1. Mwalimu Mbilo waliwaambia wanafunzi warudi nyumbani.
2. Mamvua makubwa yalinyesha na kujaza mto.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 30 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Mwalimu Sara na Mwalimu Mbilo anafundisha katika Shule ya Msingi Mtakuja.
4. Ndekia walikuwa mkaidi.
5. Mwalimu wanaishi ng'ambo ya mto.

**F. Andika sentensi hizi katika hali timilifu.**

1. Mvua kubwa inanyesha leo.
2. Wanafunzi walikwenda shuleni.
3. Maji ya mto yatakauka kwa jua.
4. Baadhi ya nyumba zilibomoka.
5. Upepo mkali utaezua paa la nyumba.

**G. Andika sentensi hizi katika wakati uliopita.**

1. Mto umejaa maji.
2. Mwalimu na wanafunzi wameshindwa kuvuka mto.
3. Wanafunzi wamekwenda shuleni baada ya mvua kukatika.
4. Maji yamezoa mazao yaliyokuwa shambani.
5. Wanafunzi wanapiga mayowe.
6. Ndekia ameshikilia tawi la mti.
7. Mwalimu Mbilo amepiga simu shuleni.
8. Mti unaoelea umekwama kwenye kizuizi.
9. Mto Zoazoa umeleta adha kwa wanakijiji.
10. Wanafunzi wamepigwa marufuku kuvuka kwenye daraja lililofunikwa na maji.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 31 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu

Majuto ni kijana mwenye umri wa miaka 15. Anaishi na wazazi wake katika Mtaa wa Mikindani. Baba yake Majuto anaitwa Mpinja na mama yake anaitwa Neema. Mzee Mpinja ni daktari katika Hospitali ya Ligula. Mama yake Majuto ni mwalimu wa Shule ya Msingi Muungano. Mzee Mpinja na mkewe wana watoto watatu; Majuto, Baraka na Upendo. Baraka na Upendo ni watoto pacha wanaosoma Darasa la Nne. Kaka yao Majuto amehitimu Darasa la Saba.

Majuto ana tabia tofauti na Baraka na Upendo. Majuto anapokuwa nyumbani hupenda kulala. Ikifika jioni huenda kuzurura. Baraka na Upendo ni wanafunzi wanaojituma wakati wote. Wanapokuwa nyumbani wanawasaidia wazazi wao kazi za nyumbani. Wazazi wao wanawapenda sana.

Tabia ya Majuto haikuwafurahisha wazazi wake. Walijitahidi kumwonya ili aache tabia mbaya lakini juhudi zao hazikuzaa matunda. Alijiunga na kundi la vijana ambao ni wezi. Aliamua kutoroka nyumbani kwao na kwenda kuishi na vijana hao. Wazazi wake walisikitika sana. Walimwambia, “Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.”

Wahenga walisema, “Siku za mwizi ni arobaini.” Siku moja Majuto na wenzake walipanga kwenda kuiba pikipiki ya kijana aitwaye Shango. Waliazima pikipiki ya rafiki yao Matata kwenda kufanya tukio hilo. Walikuwa vijana watatu. Shango hakujua kama pikipiki yake ilikuwa inawindwa na vijana hao. Mara nyingi alikuwa akisubiri abiria katika kituo cha basi. Basi lilipofika kituoni, alishuka abiria mmoja mwanamke. Mwanamke huyo alikuwa ni askari aliyevaa nguo za kiraia. Shango alipomuona

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 32 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

alimfuata na kumpakia kwenye pikipiki yake. Shango na askari huyo walikuwa wanafahamiana. Askari alimwambia ampeleke nyumbani kwake.

Kutoka kituo cha basi hadi nyumbani kwa askari ni umbali wa kilometa tano. Walipokuwa njiani Shango na abiria wake waliwaona vijana watatu wakiwa kwenye pikipiki moja. Majuto ndiye aliyekuwa akiendesha. Shango alipowakaribia aliwapita lakini Majuto alimfuata huku akiwa anaendesha pikipiki kwa kasi. Shango aliamua kusimama.

Yule askari akashuka na kuangalia kinachoendelea. Wale vijana walimvamia Shango na kumnyang'anya ufunguo wa pikipiki wakidai kuwa ni mali yao. Yule askari alipoona hivyo, akatoa **bastola** yake na kupiga risasi hewani. Shango **alipigwa butwaa** na kuanza kutetemeka.



Wezi walipoona hivyo walipanda kwenye pikipiki yao na kukimbia. Shango alipiga kelele, "Wezii! Wezi hao! Wanakimbia wako kwenye bodaboda." Wananchi waliposikia kelele waliwafukuza.



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 33 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wengine walitumia pikipiki na wengine walitumia magari. **Punde si punde** wezi **walizingirwa** na watu na kupigwa mawe na fimbo. Wezi waliumia na kupata majeraha. Askari aliwasihi watu wasiwaue badala yake aliwafunga **pingu** na kuwapeleka kituo cha polisi.

## Zoezi la 4 Ufahamu

1. Baraka na Pendo wanasoma shule gani?
2. Askari alifanya nini ili kuokoa pikipiki ya Shango?
3. Je, unapenda tabia za Majuto? Kwa nini?
4. Shango asingempakia yule askari kwenye pikipiki nini kingetokea?
5. Taja mafunzo yasiyopungua matatu yanayopatikana katika habari uliyosoma.

## Zoezi la 5 Msamiati, methali na misemo

**Oanisha maneno, methali na misemo ya sehemu A kwa kuchagua majibu kutoka sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| i. Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu. | (a) Kifaa maalumu cha chuma anachovishwa mhalifu mkononi. |
| ii. Siku za mwizi ni arobaini | (b) Jitihada hazikuleta mabadiliko yoyote. |
| iii. Punde si punde | (c) Asiyesikia ushauri wa wakubwa hupata matatizo. |
| iv. Juhudi hazikuzaa matunda | (d) Mtu mwenye tabia ya kuchukua kisicho chake bila ya ruhusa. |
| v. Pingu | (e) Mara baada ya muda mfupi. |
| vi. Mwizi | (f) Watoto wawili au zaidi waliozaliwa na mama mmoja katika uzao mmoja. |
| vii. Abiria | (g) Watoto wa baba na mama mmoja. |



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| viii. Pacha | (h) Kila ulaghai una mwisho wake iko siku ya kubainika. |
| | (i) Mtu anayetumia chombo cha kusafiria kutoka sehemu moja kwenda nyingine. |

## Zoezi la 6 Mazoezi ya lugha

### A. Andika wakati uliotumika katika kila sentensi.

***Mfano:*** *Aliondoka asubuhi na mapema - Wakati uliopita*

1. Ukiwa mwizi utapata matatizo mengi.
2. Tabia ya wizi inapaswa kukomeshwa.
3. Askari alifyatua risasi angani.
4. Nitawaeleza wenzangu kuhusu madhara ya wizi.
5. Majuto atahukumiwa kwa tabia yake ya wizi.
6. Nilimwona mwizi akiiba simu.
7. Upendo alikuwa na tabia tofauti na Majuto.

### B. Kanusha sentensi zifuatazo:

***Mfano:*** *Tabia ya wizi ni nzuri.*
*Tabia ya wizi si nzuri.*

1. Mwizi anakamatwa na watu.
2. Baraka na Upendo walinunuliwa madaftari.
3. Upendo ana tabia mbaya.
4. Wanafunzi wanaogopa mitihani.
5. Wananchi wengi walihudhuria mkutano.
6. Mbuzi atakula majani makavu.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 35 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Mavazi yetu

Katika sura hii utasoma habari kuhusu "Mavazi yetu." Utajifunza kuhusu aina mbalimbali za mavazi na kueleza mazingira yanakovaliwa. Pia, utajifunza mahali na wakati sahihi wa kuvaa mavazi hayo. Vilevile, utaweza kujua watu wanaostahili kuvaa mavazi hayo.

**Fikiri**

1. Wazazi wako hukununulia mavazi gani?
2. Ni watu gani huvaa sare?
3. Kwa nini unapokuwa nyumbani huvai sare ya shule?

## Ufahamu

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Mavazi yetu

Luko ni mwanafunzi wa Darasa la Nne katika Shule ya Msingi Kandole. Mwaka jana wakati wa likizo alikwenda kumtembelea shangazi yake jijini Dar es Salaam. Alipofika kwa shangazi yake alipokelewa vizuri.

Siku ya Ijumaa asubuhi shangazi alimwambia Luko, watakwenda kumtembelea rafiki yake aitwaye Mwageni. Shangazi alivaa gauni lenye maua ya bluu na meupe. Luko alivaa kaptura nyeusi na shati jekundu. Wakaanza safari kuelekea kituo cha **daladala**. Walipita karibu na Shule ya Msingi Kilimani. Luko

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 36 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

aliwaona wanafunzi wachache wamevaa sare. Walivaa mashati meupe, sketi na kaptura za bluu. Nyuma ya madarasa kulikuwa na viwanja vya michezo. Luko aliwaona vijana wakicheza mpira wa miguu. Walivaa **jezi** za rangi ya machungwa na wengine rangi ya zambarau. Aligundua kuwa walikuwa wakifanya mazoezi.



Walipofika kituoni, Luko aliwaona abiria wengi wakisubiri daladala. Alimwona askari aliyesimama upande wa kulia akiwa amevaa **magwanda**. Nyuma yake walisimama manesi wawili wakiwa wamevaa sare nyeupe. Walikuwa wakizungumza kwa kunong'ona. Abiria mmoja alikuwa ni mwanaume aliyevaa kanzu na baraghashia. Mwingine ni mwanamke aliyevaa **baibui** na kujifunika mtandio. Basi lilipofika, abiria wote walipanda kisha likaondoka. Ndani ya basi alikuwepo baba aliyevaa suti nyeusi na tai. Alionekana **mtanashati** sana. Mara, **utingo** aliyevaa sare ya bluu, alianza kukusanya nauli. Alipofika kwa kijana aliyesuka nywele, alikataa kutoa nauli. Utingo alimfokea kwa hasira akasema, "Bwana mdogo toa nauli. Sina utani na wewe!" Walizozana kwa muda mrefu lakini kijana hakutoa nauli. Muda wote Luko alikuwa anawashangaa. Alimuuliza shangazi, "Kwa



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 37 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nini huyo kijana hataki kutoa nauli?" Shangazi alimjibu, "Ni mkorofi, anaonekana ana hela lakini hataki kulipa. Ana tabia mbaya."

Mara ilisikika sauti ya dada mmoja, "Dereva shusha! Shusha nakwambia!" Dada huyo aliinuka kwa **madaha** na kuteremka kwenye gari. Alikuwa amevaa gauni fupi lililobana na viatu virefu. Luko alimkodolea macho na kumuuliza shangazi, "Huyu naye ni Mtanzania?" Shangazi alimjibu, "Acha tu mwanangu, **tembea ujionee, usingoje kuambiwa.**"

Baada ya nusu saa, shangazi na Luko waliteremka kwenye basi. Hatua chache mbele waliwakuta vijana wa kike na wa kiume wakicheza ngoma. Baadhi ya wasichana walivaa magauni, kanga na vitenge. Wengine walivaa sketi na blauzi za kubana. Wavulana walivaa fulana na kaptura na wengine walivaa suruali.

Dada mmoja alisikika akisema, "**Leo ni leo, asemaye kesho ni mwongo!**" Alikuwa amevaa kaptura na blauzi fupi akicheza na kurukaruka. Luko alimwangalia yule dada akashangaa na kusema, "Ama kweli mjini kuna mambo." Alimuuliza shangazi, "Mbona yule dada anacheza tumbo wazi?" Shangazi alimjibu, "Amevaa hivyo kwa sababu anacheza ngoma, ingawa alivyovaa siyo sahihi. Angeweza kuvaa nguo ndefu. Vijana wengi siku hizi huvaa mavazi yasiyo ya heshima. Wanatoa visingizio kuwa ni mitindo ya kisasa. Wao wanajiona **nadhifu** kumbe wanakosa heshima. Nguo ndefu na zenye heshima zimebaki kuvaliwa na wazee."

Baada ya muda shangazi na Luko walifika nyumbani kwa Mwageni. Walipokelewa vizuri na mwenyeji wao. Mwageni alifurahi kuwaona kwa kuwa alikuwa akiwasubiri kwa hamu. Ilipofika saa saba mchana waliandaliwa chakula kizuri. Mwenyeji wao aliwakaribisha, akasema kwa utani, "**Kaa hapa nikae pale tumfinye mchawi**." Luko na shangazi walitazamana, kisha wakatabasamu.



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 38 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Je, Luko alikwenda wapi wakati wa likizo?
2. Je, mzozo uliozuka ndani ya basi ulikuwa kati ya watu gani?
3. Nani alivaa gauni lenye maua ya bluu na meupe?
4. Luko aliwaona watu wamevaa mavazi ya aina gani?
5. Je, wanamichezo wanapokuwa kwenye mashindano huvaa mavazi ya aina gani?
6. Kwa nini Luko alimshangaa msichana aliyeteremka kwenye basi?
7. Vijana waliokuwa wanacheza ngoma walivaa mavazi gani?
8. Kwa nini Mwageni alifurahi kuwaona Luko na shangazi yake?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Chagua neno sahihi katika kisanduku kisha liandike mbele ya sentensi.**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **kanzu** | **baraghashia** | **jezi** | **sare** | **teremka** | **furahi** |
| **zozana** | **mtanashati** | **sitiri** | **nong'ona** | **magwanda** | |

***Mfano:*** *Kushuka toka ndani ya chombo cha usafiri ulichopanda. (teremka)*

1. Funika mwili kwa mavazi. ___________
2. Vazi refu linalofika miguuni linalovaliwa na wanaume. ___________
3. Nguo za kufanana zinazovaliwa na kikundi cha watu.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Kofia iliyofumwa kwa uzi wa darizi inayovaliwa na wanaume. ___________
5. Mtu mwenye tabia ya kuwa safi daima. ____________
6. Zungumza na mtu mwingine kwa sauti ya chini. ____________
7. Vazi linalovaliwa wakati wa michezo. ____________
8. Karipiana kwa maneno makali na kwa kubishana.______

## Zoezi la 3 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

1. Leo ni leo, ................
2. Samaki mkunje, ............
3. Mwenda pole,....... .....
4. Asiye na mwana,.............
5. Mtaka cha uvunguni,...........

## Zoezi la 4 Mazoezi ya lugha

**A. Andika kinyume cha sentensi zifuatazo:**

1. Ili kudumisha utamaduni wetu hatupaswi kuvaa mavazi kufuatana na jinsi.
2. Walimu wanavaa sare wanapokuwa kazini.
3. Si vizuri kuvaa mavazi ya heshima.
4. Nguo fupi husitiri mwili.
5. Mwanafunzi hodari hasomi kwa bidii.
6. Kipepeo ana rangi moja.
7. Tausi ni ndege mwenye rangi zisizovutia.
8. Wauguzi wengi huvaa mavazi meupe.



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 40 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

9. Mbwa wetu si mkali.
10. Tulisafiri kwa basi kwenda kwa bibi.

**B. Kanusha sentensi zifuatazo:**

***Mfano:*** *Msichana alivaa sketi ya kubana.*
*Msichana hakuvaa sketi ya kubana.*

1. Wakati wa likizo Luko alikwenda kwa babu yake.
2. Wanafunzi wamevaa nguo chafu.
3. Wasichana wengi watavaa nguo ndefu kwenye sherehe.
4. Askari walitembea polepole.
5. Vijana wanacheza ngoma kwa muda mrefu.
6. Siku ya Jumatatu wanafunzi wengi huhudhuria shuleni.
7. Nesi alimpa mtoto peremende kabla ya kumchoma sindano.
8. Dada anapenda kuvaa nguo fupi.
9. Wageni walipofika walipewa maji.
10. Shangazi amemkodolea macho utingo.

**C. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wakati ujao.**

***Mfano:*** *Abiria waliwahi kituoni.*
*Abiria watawahi kituoni.*

1. Wanamichezo wamevaa nguo safi.
2. Askari walishonewa magwanda mapya.
3. Vijana wanacheza mpira.
4. Dada alinunua nguo mpya.
5. Mama amevaa mavazi ya heshima.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Oanisha maneno yanayohusiana kutoka katika kundi A na B.**

| Kundi A | Kundi B |
|---|---|
| i. sare ya shule<br>ii. gwanda<br>iii. koti jeupe na kipima joto<br>iv. joho<br>v. shela | (a) dereva<br>(b) mganga<br>(c) bibi harusi<br>(d) bwana harusi<br>(e) askari<br>(f) mhitimu<br>(g) mwanafunzi |

**E. Panga maneno yaliyopo katika sentensi zifuatazo ili zilete maana.**

***Mfano:*** *Ngoma amevaa kwa sababu anacheza hivyo*
*Amevaa hivyo kwa sababu anacheza ngoma.*

1. kaptura na wavulana fulana walivaa.
2. nyeupe sketi ya kijivu blauzi na amefua.
3. sare alinunua utingo ya bluu.
4. walikula Luko na shangazi ugali.
5. nguo za kuvaa mitindo vijana hupenda.
6. mpira wanafunzi kiwanjani wanacheza.
7. sana vizuri nyimbo waliimba.
8. nauli hakutoa mkorofi kijana.

**F. Tunga sentensi kumi (10) kutokana na jedwali lifuatalo:**

| | | |
|---|---|---|
| Ndani ya gari<br>Alipokuwa barabarani<br>Walipofika kituo cha basi | alikuwemo<br>walimuona<br>waliwakuta | kijana mtanashati<br>mvulana aliyevaa jezi<br>baba aliyevaa suti<br>wauguzi wawili<br>abiria wengi |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 42 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## G. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yaliyopo kwenye kisanduku.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| mazingira | mwenyeji | walemavu | suti | mtandio |
| alifoka | abiria | ajira | amani | rushwa |
| wakinong'ona | safari | nadhifu | adui | |

***Mfano:*** *Mwenyeji wao aliwakaribisha vizuri.*

1. Mjomba wangu ni fundi hodari wa kushona ______.
2. Mama yake Asha alikuwa amejitanda ______wa bluu.
3. Juma ni kijana _______ na mwenye uwezo darasani.
4. _____ walipoingia kwenye gari utingo alikusanya nauli.
5. Baba ________ baada ya watoto kuharibu redio.
6. ________ huharibiwa kwa kukata miti ovyo kwenye vyanzo vya maji.
7. Rushwa ni ________ wa haki.
8. Serikali imezuia kutoa ________ kwa watoto.
9. Tuwapende na kutowabagua __________.
10. Shangazi alipoingia sebuleni alimsikia Luko na rafiki yake __________.

## H. Andika majina nane (8) ya mavazi kutokana na herufi zilizomo katika jedwali.

***Mfano:*** **TAI**

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | A | P | T | U | R | A | J |
| I | S | A | R | E | M | B | E |
| T | U | N | D | A | K | O | Z |
| E | S | U | R | U | A | L | I |
| N | G | U | O | G | N | P | **T** |
| G | A | U | N | I | G | I | **A** |
| E | S | U | T | I | A | A | **I** |
| U | A | F | U | L | A | N | A |



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 43 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**I. Tunga sentensi moja kwa kila aina ya mavazi yafuatayo:**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| soksi | koti | sweta | kofia | kilemba |
| tai | suruali | bukta | nepi | |

## Zoezi la 5 Vitendawili

**Tega vitendawili vyenye majibu yafuatayo:**

1. mbaazi ____________________
2. kinyonga ____________________
3. mkufu ____________________
4. mbarika ____________________
5. moto ____________________

## Zoezi la 6 Utungaji

**Fuata mwongozo ufuatao, uandike habari fupi isiyozidi maneno sitini (60) kuhusu mavazi mbalimbali.**

1. Kichwa cha habari.
2. Siku na mahali ulipokuwa unakwenda.
3. Mavazi waliyovaa watu uliokutana nao.
4. Mambo yaliyokufurahisha kuhusu mavazi ya watu hao.
5. Mambo yaliyokuudhi kuhusu mavazi ya watu hao.
6. Ushauri wako kuhusu uvaaji wa mavazi hayo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Vinywaji vyetu

Katika sura hii utasoma habari inayohusu aina mbalimbali za vinywaji. Utaweza kuelezea kwa usahihi vinywaji vyenye madhara na visivyo na madhara. Pia, utaweza kuandika habari fupi kuhusu madhara ya kutumia vinywaji vyenye kileo.

**Fikiri**

Wewe unapenda kutumia vinywaji gani? Kwa nini?

## Ufahamu

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Vinywaji vyetu

Rahatele ni mji wenye watu wengi. Katika mji huo watu wengi hupenda **starehe** na kutumia vinywaji vyenye **kileo**. Mandawa ni Bibi Afya katika mji wa Rahatele. Hakufurahishwa na baadhi ya tabia za **wakazi** wa mji huo.

Siku moja aliamua kuitisha mkutano wa kuwaelimisha watu kuhusu athari za matumizi ya vileo. Katika mkutano huo vijana na wazee walihudhuria. Alianza kwa kusema:

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 45 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Bibi Afya:** Wananchi oyee!

**Wananchi:** Oyee!

**Bibi Afya:** Leo tumekusanyika kuzungumzia suala la vinywaji vyenye kileo tunavyotumia katika mji wetu.

**Wananchi:** Sawa Bibi Afya!

**Bibi Afya:** Je, tunaweza kuvitaja vinywaji tunavyovitumia hapa kwetu?

**Mama Maua:** Vinywaji ni vingi. Tunatumia maziwa, uji, maji, **togwa** na **maji ya madafu**.

**Bibi Afya:** Vizuri mama Maua. Mwingine?

**Daudi:** Kahawa, **sharubati** na soda.

**Bibi Afya:** Asante sana. Mmetaja vinywaji vingi ambavyo vinafaa kwa afya zetu. Nani mwingine atutajie vinywaji ambavyo havijatajwa?



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 46 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maseke:** Shikamoo wakubwa! Vinywaji vingine tunavyovitumia ni mnazi, komoni, ulanzi na mbege.

**Bibi Afya:** Hivyo ndivyo haswa! Nataka tuvizungumzie. Naona Shauri umenyoosha mkono.

**Shauri:** Vingine ni pombe kali, mvinyo na bia.

**Bibi Afya:** Vizuri, vyote hivyo tutavizungumzia. Ehe! Mzee Mahanju.

**Mahanju:** Watoto wa siku hizi hawaogopi watu wazima. Wametaja aina za pombe bila wasiwasi. Mbona hawajasema bangi na dawa za kulevya wanazozitumia?

**Bibi Afya:** Mzee Mahanju, vijana wamesema ukweli, usiwalaumu. Wapo wazee na vijana wetu ambao wanatumia vinywaji vikali vyenye **madhara**. Ehe! Maseke naona umenyoosha mkono.

**Maseke:** Yote mliyosema ni kweli. Pia kunywa pombe kupita kiasi huleta umaskini.

**Bibi Afya:** Sawa kabisa Maseke. Mzee Kashamba unataka kuongezea?

**Kashamba:** Ndiyo Bibi Afya. Pia inasababisha wazazi kutengana kwa sababu ya kutokuwa na maelewano ndani ya nyumba na katika jamii.

**Maseke:** Si vinywaji vikali peke yake. Hata vinywaji vyenye sukari nyingi huleta madhara pia.

**Bibi Afya:** Ni kweli Maseke. Vinywaji vyenye sukari nyingi huongeza uzito na kusababisha meno kuoza. Hivyo basi, mnatakiwa kuwa makini na unywaji wa pombe. Pombe nyingine huandaliwa kwa kutozingatia kanuni za afya. Hivyo, huweza kusababisha mlipuko wa magonjwa.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 47 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Utumiaji wa vileo kupita kiasi unaweza kusababisha kutofanya kazi, kukosa chakula na ajali.Tujitahidi kufanya kazi kwa bidii na tusitumie vileo kupita kiasi. Tumeelewana?

**Wananchi:** Tumekuelewa Bibi Afya. Tutazingatia yote uliyotueleza.

Baadaye mkutano ulifungwa na wananchi walitawanyika. Kuanzia hapo wakazi wa mji wa Rahatele walibadili tabia zao na kufanya kazi kwa bidii.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Mandawa alikuwa anafanya kazi gani?
2. Unafikiri kwa nini Mandawa aliamua kuitisha mkutano wa wananchi?
3. Kutumia vinywaji vyenye kileo kupita kiasi husababisha madhara gani?
4. Vinywaji vyenye sukari nyingi vina madhara gani kwa binadamu?
5. Kuna faida gani za kutumia vinywaji visivyo na kileo?
6. Kama ungekuwa Bibi Afya ungewashauri nini watu wanaotumia vinywaji vyenye kileo?
7. Umejifunza nini katika habari uliyoisoma?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi moja kwa kila neno.**

| | | |
|---|---|---|
| 1. mlevi | 2. starehe | 3. madafu |
| 4. madhara | 5. athiri | 6. togwa |
| 7. wakazi | 8. sharubati | 9. kileo |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Methali na nahau

**A. Sentensi zifuatazo zimechanganywa. Kuna sentensi zenye methali na nahau. Andika neno METHALI au NAHAU kuonesha sentensi yenye methali au nahau.**

***Mfano***: *Mama alisema "Mchagua jembe, si mkulima." METHALI*

*Bahati alishika tama aliposikia kuwa Makenge amefariki kwa kileo. NAHAU*

1. Baba alisema, "Samaki mkunje, angali mbichi."______
2. Alikula kiapo cha kutekeleza kazi yake kwa uadilifu. __________
3. Mwalimu alituambia tuwe makini tunapojibu maswali kwani harakaharaka, haina baraka ________
4. Mwanafunzi mvivu humezea mate alama nzuri za wenzake. ________
5. Mara kwa mara vijana wanashauriwa kuwa hakuna marefu, yasiyokuwa na ncha. __________
6. Baada ya kushindwa mtihani Fatina alipiga moyo konde na kuamua kurudia tena mwaka unaofuata.________
7. Punde si punde Bibi Afya aliingia kwenye mkutano. ___________
8. Hadithi ya babu ilituvutia sana. Ama kweli, "Jungu kuu, halikosi ukoko." __________

**B. Kamilisha methali zifuatazo:**

1. Penye miti, ____________________
2. ______________, halimtupi mkulima.
3. Mdharau mwiba, _____________



FOR ONLINE USE ONLY

Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 49 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. ______________, utajenga ukuta.
5. Hakuna masika, ______________
6. Aisifuye mvua, ______________

## Zoezi la 4 Mazoezi ya lugha

**A. Andika NDIYO au HAPANA katika sentensi zifuatazo:**

1. Maziwa hutumika kwa watoto wachanga tu. ________
2. Sharubati ya ukwaju ni kinywaji chenye kileo. ________
3. Vimiminika ni vitu vya majimaji. ___________
4. Tunashauriwa kunywa vinywaji vyenye sukari nyingi. ______________
5. Hakuna vinywaji visivyofaa kutumiwa na binadamu. _______________
6. Wanafunzi hawaruhusiwi kutumia kileo. ____________
7. Kutumia vileo kupita kiasi husababisha umaskini. _______________.

**B. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi.**

1. Wananchi wa Rahatele anatumia sana vinywaji vyenye kileo.
2. Bibi Afya walitoa ushauri mzuri kwa wananchi.
3. Wananchi wote wanabudi kufuata maelekezo waliyopewa.
4. Kinywaji vyenye sukari sana huongeza uzito.
5. Ukitumia kileo vikali utapata madhara.
6. Mwananchi walimsikiliza Bibi Afya kwa makini.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 50 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## C. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:

***Mfano:*** *afya - dhoofu*

1. mbele ____________
2. umaskini ____________
3. kosa ____________
4. dharau ____________
5. kaidi ____________
6. nyooka ____________

## D. Pigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine.

1. sabuni, mnazi, ulanzi, mbege.
2. maziwa, soda, sharubati, chungwa.
3. daktari, nesi, bibi afya, mkulima.
4. baba, mama, chakula, mtoto.
5. ugali, tumbo, kichwa, mabega.
6. mazao, wananchi, wakazi, watu.

## E. Chunguza jedwali lifuatalo kisha, andika vinywaji sita (6) visivyo na kileo.

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | I | A | J | U | I | S | I | T |
| M | A | Z | I | W | A | F | S | O |
| A | S | A | L | I | B | CH | O | G |
| J | O | T | O | K | A | A | D | W |
| I | K | O | M | O | N | I | A | A |

## F. Tunga sentensi sita (6) kwa kutumia jedwali lifuatalo:

| | | |
|---|---|---|
| Wanafunzi<br>Wagonjwa<br>Vijana<br>Watoto | hawaruhusiwi | kutumia vinywaji vyenye vileo<br><br>kutumia vyakula vyenye sukari nyingi |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5 Utungaji

**Kamilisha habari kuhusu vinywaji kwa maneno yasiyopungua hamsini (50). Zingatia yafuatayo:**

1. Maana ya vinywaji.
2. Aina za vinywaji.
3. Vinywaji visivyo na kileo na vyenye kileo.
4. Madhara ya kutumia vinywaji vyenye kileo.

Vinywaji ni vitu vya majimaji vinavyonywewa kama uji, chai, maziwa, soda na togwa. Vinywaji hivi havina kileo. Vipo vinywaji vingine vyenye kileo kama .................................

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 52 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Mimea yetu

Katika sura hii utasoma majigambo yanayohusu mimea. Utaweza kueleza aina mbalimbali za mimea na faida zake kwa ufasaha. Vilevile, utaweza kuandika habari fupi kuhusu mimea.

**Fikiri**

1. Taja mimea unayoifahamu.
2. Mimea ina faida gani kwa binadamu?

FOR ONLINE USE ONLY

## Ufahamu

*Soma majigambo yafuatayo, kisha jibu maswali.*

### Mimea yetu

**Mbuyu:** Mimi ni Mbuyu, ni mti mkubwa kuliko miti yote. Nina shina kubwa ambalo haliwezi kukatika kwa urahisi. Matunda yangu hutoa mbegu zenye faida nyingi kwa binadamu. Matunda haya hutoa unga unaotengenezea juisi. Juisi hiyo huimarisha meno na mifupa ya binadamu. Mbegu zangu zikitiwa rangi na sukari huleta ladha nzuri. Pia hutumika kutengenezea mafuta ya kupaka mwilini. Majani yangu laini hutumika kama mboga. Mimi ninawavutia **watalii** wanaotembelea nchi yetu. Mimi ni chanzo cha mapato. Ama kweli, nina faida nyingi.



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 53 7/23/21 2:59 PM



**Mkahawa:** Mimi ni Mkahawa. Unaweza kuniita mbuni. Ninastawi sehemu zenye baridi. Ninazaa matunda yaitwayo kahawa au buni. Matunda yangu husagwa na hutengenezea kinywaji cha moto kiitwacho kahawa. Unga wangu hutengenezea peremende na chokoleti. Ninaongeza ladha na harufu nzuri katika bidhaa hizi. Bidhaa ninazotoa huuzwa ndani na nje ya nchi. Watu hutafuna mbegu zangu kwa ajili ya kujiburudisha. Kwa ujumla nina faida nyingi sana. Ukinikata utasababisha kuporomoka kwa uchumi wa nchi.





FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mkorosho:** Mimi ni Mkorosho. Ninaishi kwa muda mrefu. Nina faida kubwa sana. Ninazaa mabibo na korosho ambayo huliwa na binadamu. Mabibo yangu hutengenezea juisi na korosho huliwa. Hupendwa sana na binadamu. Korosho zangu ni zao la biashara. Huuzwa ndani na nje ya nchi. Matawi yangu yakikauka hutumika kama kuni. Mimi ni chanzo cha mapato. Kwa ujumla, nina faida kubwa sana. Ukinikata utapata hasara.



## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Katika habari uliyosoma kuna mmea upi unaotoa zao linalolinda meno na mifupa?
2. Mabibo huzaliwa na mti gani?
3. Mafuta ya kupaka yanapatikana katika mbegu za mmea gani?
4. Mmea upi unastawi katika hali ya baridi?



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Unga wa mmea gani huongeza harufu na ladha nzuri katika bidhaa?
6. Ni mmea gani ambao ulisema ukikatwa kutatokea hasara?
7. Kuna umuhimu gani wa kuhifadhi mimea katika mazingira yetu?
8. Umejifunza nini kutokana na majigambo uliyosoma?

## Zoezi la 2 Kazi ya kufanya

**Igiza na mwenzako majigambo uliyosoma.**

## Zoezi la 3 Nahau

**Tunga sentensi moja kwa kila nahau zifuatazo:**

***Mfano:*** *Kitendo cha kuacha ng'ombe waharibu mazao, kiliwavunja moyo wakulima.*

1. piga marufuku
2. mezea mate
3. piga mbiu
4. unga mkono
5. ona haya

## Zoezi la 4 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

1. ____________________, hupata koroma.
2. Jogoo wa shamba, ____________________.
3. ____________________, si mkulima.
4. Dau la mnyonge,____________________.
5. ____________________, mguu huota tende.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 56 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **mboga** | **matunda** | **mbolea** | **mmea** |
| **mkahawa** | | | |

1. __________ ni kitu chenye uhai, majani, shina na mizizi kinachoota kutokana na mbegu au tawi.
2. Buni ni tunda linalopatikana katika mti wa___________.
3. ____________ni mboji na samadi.
4. Mapapai, mapera, matango na zabibu ni___________.
5. ________ ni majani yanayoliwa na binadamu baada ya kupikwa.

**B. Oanisha mmea uliopo katika sehemu A na zao lake katika sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| i. mchungwa | (a) korosho |
| ii. mhogo | (b) mapera |
| iii. mpapai | (c) maembe |
| iv. mbaazi | (d) katani |
| v. mstafeli | (e) pilipili |
| vi. mpera | (f) machungwa |
| vii. mkonge | (g) mapapai |
| viii. mpilipili | (h) stafeli |
| ix. mkorosho | (i) kisamvu na mihogo |
| x. mwembe | (j) mbaazi |



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 57 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika NDIYO au HAPANA.**

1. Mimea ni sehemu ya mazingira. ____________
2. Mimea haina faida kwa binadamu. ___________
3. Simba, chui na mbwamwitu hula majani. __________
4. Mimea jamii ya kunde ina faida kwa binadamu. ________
5. Baadhi ya mimea ni dawa. _____________
6. Mboga za majani hulinda na kujenga mwili. __________

**D. Panga vizuri herufi ili kupata jina la mmea.**

***Mfano:*** *mumbazara - mzambarau*

| | | |
|---|---|---|
| chamchi | gombam | zimna |
| chungwam | olimam | paimpa |

**E. Soma orodha ya maneno hapa chini. Orodhesha majina ya mimea katika safu A na yasiyo ya mimea safu B.**

**Mfano:**

| Safu A (mimea) | Safu B (si mimea) |
|---|---|
| mchicha | maji |
| mninga | sabuni |

mbaazi, mlingoti, ubao, mkonge, mchaichai, mstafeli, ngamia, mnazi, nanasi, mwembe, boga, bata, mualizeti, magamba, muwa, mabati, mgomba, mchungwa, umande, mtopetope.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**F. Chagua neno kutoka kwenye mabano lenye maana sawa na sentensi ulizopewa.**

1. Eneo ambalo wanasiasa husimama wakitoa hotuba.
   __________ (kizimbani, mimbari, jukwaa)
2. Mafuta mazito ya kupaka kwenye mkate.
   _________ (mtindi, siagi, makaroni)
3. Uwezo wa kutoa ushauri kusuluhisha mgogoro baina ya watu wawili.__________
   (ubabe, busara, msaada)
4. Uuzaji wa vitu kwa kushindanisha bei hadharani.
   __________(shindano, gulio, mnada)
5. Eneo linalobubujika maji kutoka ardhini. _________
   (kisima, chemchemi, chekecheo)

**G. Chunguza picha ifuatayo kisha jibu maswali.**



FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 59 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Zizi la ng'ombe lipo __________ ya nyumba.
2. Baba na mama wamekaa __________ ya mti.
3. Mti upo __________ ya nyumba.
4. Watoto wako __________ ya nyumba.
5. Ndege wanaruka __________ ya mti.

## Zoezi la 6 Utungaji

**Chunguza picha ifuatayo kisha malizia habari uliyopewa kwa maneno yasiyozidi hamsini (50).**



Mimi ni ..............................., ninajivunia majani yangu ya rangi ya kijani iliyokolea. Majani yangu huitwa ..................................., mboga inayopendwa na kuliwa na watu wengi. .................................

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 60 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Zahanati yetu

Katika sura hii utasoma habari inayohusu zahanati. Utajifunza kuhusu vifaa vinavyopatikana katika zahanati na huduma zinazotolewa. Utaweza kuandika habari fupi kuhusu umuhimu wa zahanati.

**Fikiri**

Je, watu huenda zahanati kufanya nini?

## Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Zahanati yetu

Hamidu anasoma Darasa la Nne katika Shule ya Msingi Mazoea. Mwalimu wao wa somo la Sayansi anaitwa Paulo. Siku ya Jumatatu mwalimu Paulo aliingia darasani. Wanafunzi walisimama na kumsalimia lakini Hamidu alijilaza kwenye dawati. Mwalimu alipomwona aliuliza, "Kwa nini Hamidu hujasimama?" Rehema kiongozi wa darasa alijibu, "Anaumwa." Mwalimu alimsogelea Hamidu na kumgusa kwenye shavu. Aligundua kuwa alikuwa na joto kali sana. Alimshika mkono na kwenda naye ofisini.

Alipofika ofisini, walimu wenzake walimshauri ampeleke Hamidu zahanati. Hamidu aliposikia hivyo alianza kulia. Mwalimu Paulo alishangaa, akamuuliza, "Unalilia nini?"

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hamidu akajibu, “Usinipeleke zahanati watanichoma sindano.” Mwalimu akatabasamu akamwambia, “Usiogope, jipe moyo hawatakuchoma sindano.”

Hamidu na mwalimu waliondoka kwenda zahanati. **Punde si punde** walifika zahanati na kuingia kwa **tabibu**. Tabibu alipomwona mwalimu Paulo alimuuliza kwa mshangao, “Ah kaka! Una tatizo gani?” Mwalimu Paulo akajibu, “Mwanafunzi wangu Hamidu anaumwa.” Tabibu aliwakaribisha kisha akamuuliza Hamidu, “Unajisikiaje?” Hamidu akamjibu, “Ninaumwa kichwa.” Tabibu alimwangalia usoni kisha akamwekea **kipimajoto** kwapani. Baada ya dakika tatu alikitoa na kukitazama. Akaandika katika kadi huku akisema, “Ni kweli joto lake liko juu.” Akachukua karatasi nyingine akaandika na kuwaelekeza waende **maabara** kwa ajili ya vipimo.

Walipoingia chumba cha maabara walimkuta mtaalamu wa maabara. Mtaalamu alichukua kisindano kidogo na kumwambia Hamidu, “Leta mkono.” Akamchoma kidole cha katikati na kumtoa damu kisha akaipakaza kwenye kioo kidogo. Alipomaliza aliweka kioo hicho kwenye **hadubini** ili kuchunguza damu. Akawaambia wakasubiri nje.

Wakiwa wanasubiri, Hamidu aliweza kuona kupitia dirisha kubwa la maabara. Alimwona mtaalamu akitazama kwenye hadubini. Mtaalamu aliandika majibu ya vipimo kwenye karatasi. Aliwaambia wairudishe kwa tabibu. Tabibu aliisoma akasema, “Ana malaria.” Akamuandikia dawa.

Kabla hawajaondoka, mwalimu Paulo alimwomba tabibu kwenda kutembelea shule yake. Alitaka akawaeleze wanafunzi umuhimu wa zahanati. Tabibu alikubali na kuahidi kwenda siku ya Alhamisi.

Siku ilipofika tabibu aliwasili shuleni. Mwalimu Paulo alimtambulisha kwa walimu kisha wakaingia darasani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wanafunzi walisimama wakamsalimia mgeni na mwalimu wao. Mwalimu Paulo alimtambulisha mgeni kuwa anaitwa Asha na ni tabibu. Aliwaeleza wanafunzi kuwa tabibu amewatembelea kwa lengo la kuwaeleza umuhimu wa zahanati. Wanafunzi walifurahi sana.



Tabibu aliwaeleza wanafunzi kuwa tunapojisikia dalili za ugonjwa inatupasa kwenda zahanati. Si vizuri kutumia dawa kabla ya kupata vipimo. Tabibu ndiye atakayekushauri dawa ya kutumia baada ya kujua ugonjwa wako. Tabibu aliendelea kwa kuwatajia wanafunzi vifaa mbalimbali vinavyotumika zahanati. Alivitaja vifaa hivyo kuwa ni kipimajoto ambacho hutumika kupima joto la mwili.

Alitaja kifaa kingine kuwa ni hadubini. Alieleza kuwa hadubini ni kifaa cha kukuza vitu vidogo visivyoonekana kwa macho. Pia, alitaja kifaa cha kupima mapigo ya moyo na mapafu. Vifaa vingine alivyovitaja ni wembe, mkasi, **bandeji** na sindano.



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 63 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kila alipotaja kifaa husika aliwaonesha wanafunzi. Tabibu alieleza kuwa kuna vifaa vingine kama beseni na ndoo ambazo hakuweza kuja navyo darasani.

Baada ya kutaja vifaa vinavyotumika zahanati, tabibu alitaja huduma zinazotolewa zahanati. Alizitaja kuwa ni kumpima mgonjwa, kumpatia dawa mgonjwa inayostahili na kutoa ushauri. Alieleza kuwa vipimo vingine ni vya haja kubwa na ndogo. Vilevile, alitaja huduma ya kwanza inayotolewa kwa wagonjwa wanaohitaji msaada wa haraka.

Mwisho aliwasisitiza wanafunzi kusoma kwa bidii kwani **elimu ni bahari**. Tabibu aliwashukuru wanafunzi kwa kumsikiliza kisha aliwaaga.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Habari uliyoisoma inahusu nini?
2. Mwalimu Paulo alikuwa anafundisha somo gani?
3. Hamidu na mwalimu walikwenda wapi?
4. Kwa nini Hamidu alilia alipoambiwa anapelekwa zahanati?
5. Nani alimpima Hamidu?
6. Huduma gani hutolewa katika zahanati?
7. Zahanati kuna vifaa gani?
8. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 64 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi moja kwa kutumia maneno yafuatayo:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| kipimajoto | vipimo | tabibu | maabara |
| tiba | zahanati | pakaza | hadubini |

## Zoezi la 3 Mazoezi ya lugha

**A. Chagua jibu lililo sahihi, kisha andika herufi yake katika kisanduku.**

1. Tabibu aliwashauri wanafunzi;
   (a) kuacha michezo
   (b) kusoma kwa bidii
   (c) kuwasaidia wazazi
   (d) kupendana

2. Tunapotaka kupata huduma;
   (a) tuombe msaada
   (b) tutoe rushwa
   (c) tukae kimya
   (d) tuvumilie

3. Tabibu pia anaweza kuitwa;
   (a) mwalimu
   (b) mganga
   (c) msaidizi
   (d) mponyaji

4. Tunaboresha mazingira kwa;
   (a) kukata miti
   (b) kurundika takataka
   (c) kupanda miti
   (d) kufuga mifugo katika eneo moja

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Tunapokuwa na dalili za ugonjwa;
   (a) tumeze dawa
   (b) tupime joto
   (c) tuchome sindano
   (d) twende zahanati

**B. Andika sentensi zifuatazo kwa mfuatano sahihi ili kuunda kifungu cha habari.**

1. Hamidu hakusimama.
2. Hamidu alipelekwa zahanati.
3. Alipoingia darasani wanafunzi walisimama na kumsalimia.
4. Mwalimu alimgusa Hamidu akagundua ana joto kali.
5. Mwalimu aliuliza, “Kwa nini Hamidu hakusimama?”
6. Mwalimu Paulo anafundisha somo la Sayansi.
7. Rehema alimwambia mwalimu kuwa Hamidu anaumwa.

**C. Andika maneno mapya mawili kutokana na herufi na silabi za maneno uliyopewa.**

***Mifano:***

*(a) chungulia – chunga, lia.*

*(b) mkulima – kuli, lima.*

*(c) unganisha – unga, ushanga.*

1. popoa ........................
2. rudisha ........................
3. tendea ........................
4. tekenya ........................
5. azima ........................

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. umia ………………..
7. pumbaza ………………..
8. chechemea ………………..
9. mtundu ………………..
10. tabibu ………………..

**D. Oanisha maneno ya sehemu A na maana zake kutoka sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| i. hadubini | (a) karatasi ngumu ya kuandikia |
| ii. zahanati | (b) tia kitu cha majimaji kwenye kitu kingine |
| iii. maabara | (c) kifaa chenye lenzi cha kupimia viumbe hai wadogowadogo wasioonekana kwa macho |
| iv. pakaza | (d) jengo au chumba cha kufanyia uchunguzi wa magonjwa |
| v. kadi | (e) mahali ambapo huduma ya matibabu hutolewa |
| vi. kwapa | (f) sehemu iliyo chini ya bega la binadamu |
| vii. sindano | (g) kifaa cha tiba, chembamba na chenye ncha kinachotumika kuingiza dawa kwenye mwili wa mtu au mnyama |
| viii. vipimo | (h) uchunguzi wa kitaalamu unaofanywa ili kujua kiwango cha wadudu wa maradhi |
| ix. koleo | (i) chumba cha kulaza wagonjwa |
| | (j) kiwiko cha mkono wa kushoto |
| | (k) kifaa kinachotumika kutolea meno |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Andika umoja na wingi wa maneno yafuatayo:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| i. kipimo | ................................. |
| ii. ................................. | magonjwa |
| iii. zahanati | ................................. |
| iv. ................................. | hadubini |
| v. kifaa | ................................. |
| vi. muuguzi | ................................. |
| vii. ................................. | vyumba |

**F. Andika sentensi zifuatazo katika wakati ujao.**

1. Tabibu aliwafundisha umuhimu wa zahanati.
2. Wanafunzi walifanya ziara ya kimasomo.
3. Alitumia hadubini kufanya uchunguzi.
4. Rehema alimpokea mgeni shuleni.
5. Mwalimu Paulo anafundisha somo la Sayansi.
6. Asha anaongea na wanafunzi wote.
7. Tulisafisha mazingira ya shule.
8. Baraka alisoma shairi.

**G. Tunga sentensi mbili kwa kutumia vifungu vya maneno vifuatavyo:**

1. punde si punde
2. jipe moyo
3. elimu ni bahari

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 68 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**H. Jaza herufi zinazolingana na namba hizi ili kupata maneno yanayotumika zahanati.**

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | B | CH | D | E | F | G | H | I | J | K | L | M | N | O | P | R |

| 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | T | U | V | W | Y | Z |

***Mfano:***

| 11 | 9 | 4 | 15 | 14 | 4 | 1 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| K | I | D | O | N | D | A |

**1.**

| 13 | 11 | 1 | 18 | 9 |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

**2.**

| 13 | 20 | 20 | 7 | 20 | 24 | 9 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |

**3.**

| 2 | 5 | 18 | 5 | 14 | 9 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

**4.**

| 18 | 9 | 14 | 4 | 1 | 14 | 15 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |

**5.**

| 8 | 1 | 4 | 20 | 2 | 9 | 14 | 9 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 69 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6.

| 24 | 1 | 8 | 1 | 14 | 1 | 19 | 9 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |

7.

| 19 | 1 | 2 | 9 | 2 | 20 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

8.

| 21 | 9 | 16 | 9 | 13 | 15 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

## Zoezi la 4 Utungaji

**Andika habari fupi isiyopungua maneno sitini (60) kuhusu umuhimu wa zahanati.**

Maswali yafuatayo yatakuongoza:

1. Kwa nini watu wanakwenda zahanati?
2. Watu gani hutoa huduma zahanati?
3. Wagojwa wanapofika zahanati hupata huduma gani?
4. Vipimo gani ambavyo wagonjwa hupimwa wanapokwenda zahanati?

**Anza hivi:** Zahanati ni mahali wanapokwenda wagonjwa kupata matibabu............

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 70 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Kazi zinazofanyika kila siku

Sura hii itakuwezesha kueleza kazi zinazofanyika kila siku kwa kuzingatia nyakati. Utaweza kuandika ratiba juu ya shughuli za kila siku katika nyakati mbalimbali.

**Fikiri**

1. Shughuli zipi zinafanyika nyumbani kila siku?
2. Unafanya kazi gani kabla ya kwenda shuleni?
3. Unafanya kazi gani unapoamka asubuhi siku za mapumziko?

## Ufahamu

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Juhudi na Amani

Juhudi anasoma Darasa la Nne katika Shule ya Msingi Upendo. Kaka yake anaitwa Amani na anasoma Darasa la Sita. Siku ya Jumapili Juhudi aliamka asubuhi na mapema. Alianza kuosha vyombo huku akiwa anaimba wimbo wa "Tanzania Nakupenda." Alipomaliza alifagia uwanja na kupiga deki.

Amani alipoamka alimsalimia Juhudi kisha alikwenda kwenye zizi la ng'ombe. Alimkamua ng'ombe na kupeleka maziwa jikoni. Baada ya hapo alikwenda kusafisha banda la mbwa. Alipomaliza aliendelea na shughuli nyingine za bustani. Juhudi alitayarisha chai na kuandaa meza.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 71 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Ilipofika saa 2:00 asubuhi, Zawadi alifika nyumbani kwa akina Juhudi. Alibisha hodi.

**Zawadi:** Hodi!

**Juhudi:** Karibu! Karibu rafiki yangu, ingia ndani. Hujambo?

**Zawadi:** Asante, mimi sijambo.

**Juhudi:** Karibu chai. Jana nilikusubiri sana sikukuona.

**Zawadi:** Asante, nimeshakunywa. Jana niliamka saa 12:00 asubuhi nikaenda shambani kupalilia mahindi. Niliporudi muda wa saa 6:00 mchana nilikwenda kuchota maji. Baadaye nilifanya usafi wa nyumba na kufua nguo. Saa 10:00 jioni nilikwenda bustanini kuchuma mboga. Niliporudi nilimsaidia mama kuosha vyombo.

**Juhudi:** Hongera sana. Hivi huja**tia chumvi**! Unaweza kulima kweli?

**Zawadi:** Ndiyo. Naweza sana! Kwani unanionaje?

**Juhudi:** Aka! Sikatai! Kumbe ratiba yako kidogo inafanana na yangu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zawadi:** Tuache hayo bwana! Leo nimekuletea daftari lako kwani **ahadi ni deni**. Sasa naomba niondoke.

**Juhudi:** Mbona una haraka?

**Zawadi:** Aaah! Acha niende bwana, unapenda niendelee **kupiga domo**? Nitakuja siku nyingine.

Zawadi aliondoka kuelekea nyumbani kwao na Juhudi aliendelea na kazi zake. Aliosha vyombo vya chai, alifua na kupika chakula cha mchana. Nguo zilipokauka alizianua na kuzinyoosha. Juhudi alikuwa ni mtoto hodari na mchapakazi. Ama kweli, **wingi si hoja**. Mara zote Juhudi alimudu kufanya kazi nyingi peke yake.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Rafiki wa Juhudi aliitwa nani?
2. Amani alifanya shughuli zipi siku ya Jumapili?
3. Amani alifanya nini baada ya kukamua maziwa?
4. Kwa nini Zawadi alichelewa kupeleka daftari kwa Juhudi?
5. Kuna umuhimu gani wa kusafisha mabanda ya mifugo?
6. Umejifunza nini kuhusiana na habari hii?

## Zoezi la 2 Miundo

**Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.**

***Mfano:*** *Anapenda kuimba kila siku anapokuwa shambani.*

1. .................. kila wakati....................
2. ................ huku na huko.......................
3. ..............mara kwa mara....................
4. ................ kila siku.....................
5. Kila mara.......................

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 73 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Nahau

**Eleza maana ya nahau zifuatazo:**

***Mfano:*** *Paka mafuta kwa mgongo wa chupa*
*Kumpa mtu sifa asizostahili.*

1. tia fora
2. tia moyo
3. tia chumvi
4. tia nanga
5. tia doa

## Zoezi la 4 Mazoezi ya lugha

**A. Chagua jibu lililo sahihi, kisha andika herufi yake katika kisanduku.**

1. Zawadi alisema, "Unapenda niendelee kupiga domo?" maana yake ni:
   (a) kuropoka
   (b) kuongea
   (c) kusengenya
   (d) kupiga mdomo

2. Methali ya "Wingi si hoja" inafanana na methali ipi?
   (a) Kidole kimoja, hakivunji chawa.
   (b) Ndondondo si, chururu.
   (c) Ukubwa wa pua, si wingi wa kamasi.
   (d) Haba na haba, hujaza kibaba.

3. Ahadi ni deni maana yake ni nini?
   (a) Ukiahidi jambo lazima ulitekeleze.
   (b) Ukikopa utadaiwa.
   (c) Madeni hulipwa kwa ahadi.
   (d) Haifai kuwa na deni.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 74 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Nini maana ya kuandaa meza?
   (a) Kupanga vizuri meza.
   (b) Kutayarisha chakula mezani.
   (c) Kupamba meza.
   (d) Kutandika kitambaa mezani.

5. Katika habari hii neno zizi lina maana gani?
   (a) Mzizi unaoota karibu na nyumba.
   (b) Sehemu inayouziwa ng'ombe.
   (c) Sehemu inayoogeshewa ng'ombe.
   (d) Boma lililojengwa kwa ajili ya ng'ombe.

## B. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wakati uliopo.

***Mfano:*** *Mzee Azizi atakwenda Unguja kwa mwanawe.*
*Mzee Azizi <u>anakwenda</u> Unguja kwa mwanawe.*

1. Wanafunzi wa Darasa la Nne walifagia darasa lao.
2. Mwalimu aliingia darasani mapema.
3. Roza atafurahia kuwaona wanafunzi wenzake.
4. Wageni wameondoka leo.
5. Amani atajikumbusha alichosoma darasani.
6. Juhudi alifagia uwanja.
7. Amani atapalilia bustani ya mboga.
8. Kaka alifanya kazi kwa bidii.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 75 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## C. Chunguza picha zifuatazo kisha jibu maswali haya.

Taja aina ya kazi na shughuli za watu hawa.

***Mfano:*** *Mwalimu - kufundisha*

a



b



c



d



e



f





Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 76 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

g


h


**D.** **Tunga sentensi kwa kutumia maneno ya sehemu A na B ili kukamilisha maana.**

***Mfano:*** *Nyoka <u>mweusi</u> aliingia kwenye <u>shimo</u>.*

| Na. | Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|---|
| i. | nyoka | shimo |
| ii. | kuku | totoa |
| iii. | mbwa | kibanda |
| iv. | ng'ombe | maziwa |
| v. | sufuria | chakula |
| vi. | chota | maji |
| vii. | mto | tiririka |
| viii. | moto | unguza |

**E.** **Andika sentensi zifuatazo katika wakati uliopita.**

***Mfano:*** *Anatandika kitanda chake vizuri.*
*<u>Alitandika</u> kitanda chake vizuri.*

1. Umetambuaje maneno hayo?
2. Ameketi mezani kupata kifunguakinywa.



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 77 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Nani atamzawadia Sauda?
4. Jafari ameona garimoshi.
5. Tutamtembelea rafiki yetu Jumapili.
6. Neema atatoa taarifa ya safari yao.
7. Jogoo anawika alfajiri.
8. Miti ya matunda imepandwa kwenye bustani ya shule.

## F. Imba wimbo ufuatao kisha jibu swali.

**Wimbo**

*Watoto wenye ulemavu*
*Wasibaguliwe x 2*

*Shida za wenye ulemavu*
*Zitatuliwe x 2*

*Haki za wenye ulemavu*
*Zitambuliwe x 2*

*Vipaji vya wenye ulemavu*
*Viendelezwe x 2*

**Swali**

Wimbo huu unakufundisha nini?

## G. Onesha nyakati katika sentensi zinazofuata.

***Mfano:*** *Dada atakwenda Arusha wakati wa likizo.*
*(Wakati ujao)*

1. Tunashirikiana kufanya kazi.
2. Kaka alijenga uzio wa kuzuia kuku wasitoke bandani.
3. Mpoki alipanda mabasi ya mwendokasi.
4. Mtete anapanda gari la alfajiri kila mara.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 78 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Mgonjwa ataruhusiwa kesho jioni.
6. Mama atatupikia kisamvu na ugali wa dona.
7. Matola anaweza kucheza mpira wa pete.
8. Watoto walikimbilia darasani mvua kubwa ilipoanza kunyesha.
9. Baba atarina asali yetu wiki ijayo.

## Zoezi la 5 Vitendawili

**Chunguza picha zifuatazo kisha tunga vitendawili.**

a



b



c



d



e



f



## Zoezi la 6 Utungaji

**Andika ratiba yako ya siku nzima ya Jumamosi ukionesha muda.**



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 79 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

## Kutumia alama za uandishi

Katika sura hii utasoma hadithi ya "Ndoto yangu." Utaweza kueleza ujumbe na mafunzo yaliyomo katika hadithi hiyo. Pia, utaweza kusikiliza, kusimulia hadithi na kueleza ujumbe uliomo. Vilevile hadithi hii itakuwezesha kuandika sentensi kwa kuzingatia alama za uandishi.

**Fikiri**

Je, unaposoma habari au hadithi unapaswa kuzingatia nini?

## Ufahamu

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Ndoto yangu

Ilikuwa ni wakati wa usiku. Siku hiyo kulikuwa na mvua kubwa iliyoambatana na radi. Nilikuwa chumbani kwangu nikisoma kitabu cha hadithi. Mara nilimsikia baba akiniita, "Mboni! Mboni! Zima taa ulale, kuna radi sana." Nilijiuliza hivi kuna uhusiano gani kati ya radi na taa? Nilizima taa nikalala.

Baada ya muda mfupi **nililala fofofo** nikaota ndoto. Ndoto hiyo ilikuwa nzuri sana. Niliota kuwa tumekwenda Zanzibar kutembelea makumbusho. Tulipokuwa huko tulikwenda Forodhani kuona Jumba la Mfalme. Tulipoingia ndani tukaona vitu mbalimbali vya kale. Tuliona vitu kama visu, mapanga, sarafu, mbuzi za kukunia nazi na majiko ya asili. Vilevile, tuliona samani kama vitanda vyenye **besera** na magodoro



FOR ONLINE USE ONLY

Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 80 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ya sufi. Baadaye tulikwenda Mkunazini ambako kulikuwa na Soko la Watumwa. Huko tuliona picha mbalimbali za watumwa waliofungwa minyororo.

Baada ya kutoka Mkunazini tulikwenda Kisiwandui. Tuliona kaburi la Rais wa kwanza wa Zanzibar, Shekhe Abeid Amani Karume. Mimi na wanafunzi wenzangu tulipiga picha mbalimbali za ukumbusho. Wakati wote huo nilikuwa usingizini. Kwa mbali nilisikia sauti, "Mboni! Mboni! Kumekucha amka ujiandae kwenda shule."Mama aliniita. Niliamka haraka na kwenda kupiga mswaki kisha nikaoga na kuvaa sare ya shule. Mama aliniandalia **kifunguakinywa**. Baada ya kupata kifunguakinywa nilikwenda shuleni. Nilipofika shuleni niliwasimulia wanafunzi wenzangu kuhusu ndoto yangu. Wote walivutiwa na ndoto hiyo. Kengele ilipogongwa tuliingia darasani.

Mwalimu wa somo la Maarifa ya Jamii aliingia darasani. Alitueleza kuwa tutakuwa na ziara ya kutembelea mapango ya Amboni. Mapango hayo yako katika mkoa wa Tanga. Mwalimu ali**toa wosia** kwa wanafunzi kabla ya kuondoka, kuwa watulivu watakapokuwa mapangoni. Sikuamini masikio yangu! Nilikumbuka ndoto yangu. Wanafunzi wote walifurahi sana kwani waliweza ku**kata kiu** yao kwa kutembelea mapango ya Amboni.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Kwa nini baba yake Mboni alimwambia Mboni azime taa?
2. Kama mama yake Mboni asingemuamsha Mboni nini kingetokea?
3. Mboni aliona nini kwenye Jumba la Mfalme katika ndoto yake?
4. Je, vitu gani ambavyo unafikiri vinaweza kuwekwa kwenye makumbusho?
5. Makumbusho yana umuhimu gani?
6. Eleza mambo mawili muhimu uliyojifunza kutokana na hadithi uliyoisoma.
7. Simulia hadithi uliyoisoma kwa maneno yako.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kila neno.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) radi | (b) kale | (c) makumbusho | (d) ndoto |
| (e) watumwa | (f) ziara | (g) minyororo | (h) sufi |

## Zoezi la 3 Nahau

**Tunga sentensi mbili kwa kila nahau zifuatazo:**

1. lala fofofo
2. kata kiu
3. toa wosia

## Zoezi la 4 Mazoezi ya lugha

**A. Oanisha maneno ya kifungu A na maana zake kutoka kifungu B.**

| Kifungu A | Kifungu B |
|---|---|
| i. radi | (a) zamani |
| ii. lala fofofo | (b) mlo wa asubuhi anaokula mtu kabla ya kula kitu kingine chochote |
| iii. sarafu | (c) sauti kubwa inayotoka mawinguni inayoambatana na mwanga mkubwa wakati wa mvua |
| iv. watumwa | (d) viguzo vya mbao au chuma vinavyoungwa kwenye pembe za kitanda ili kutundikia chandarua |
| v. kale | (e) fedha |
| vi. besera | (f) lala usingizi mzito. |
| vii. kifunguakinywa | (g) watu wanaotumikishwa na watu wengine bila ridhaa yao wala malipo yoyote |
| | (h) chombo cha kuogea |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Andika NDIYO au HAPANA katika sentensi zifuatazo:**

1. Ndoto ni maono yatokeayo usingizini..................
2. Si vema kuzima taa inaponyesha mvua inayoambatana na radi...............
3. Vitu vinapowekwa kwa ajili ya makumbusho huongeza pato la taifa............
4. Mambo ya kale yamepitwa na wakati hayapaswi kufundishwa tena............
5. Rais wa kwanza wa Zanzibar ni Shekhe Amri Abeid ................

**C. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

1. usiku ____________
2. zima ____________
3. lala ____________
4. furaha ____________
5. ingia ____________

**D. Andika aya ifuatayo kwa usahihi kwa kuzingatia alama za uandishi.**

paulina ni mwanafunzi wa darasa la nne anapenda kusoma na rafiki zake mboni baraka na tumaini wakati wa kufunga shule alitangazwa kuwa mshindi wa kwanza katika darasa lao alishtuka na kusema aha nimewashinda wote ndoto ya paulina ni kusoma hadi chuo kikuu na kuwa rubani paulina ni mwanafunzi anayejitambua na mwenye kuweka malengo ya baadaye wewe je

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 83 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuchagua neno sahihi kutoka kwenye kisanduku.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| tulipokuwa | walipokuwa | nilipokuwa | kilipokuwa |
| alipokuwa | zilipokuwa | vilipokuwa | mlipokuwa |

***Mfano:*** *<u>Ulipokuwa</u> mdogo ulikuwa mnene.*

1. ___________ nimelala niliota ndoto.
2. Baba _______ anasoma alidondosha miwani yake.
3. Wanafunzi ________ shuleni mlifanya bidii katika masomo yenu.
4. Tulipiga picha za ukumbusho __________ Mkunazini.
5. Vikombe vilivunjika _____________ vinaoshwa.
6. Nyaya ziliunganishwa ___________ zimekatika.
7. Kipindi __________ kinaendelea wanafunzi wengine walikuwa wanacheza.
8. Wanafunzi _________ katika Jumba la Mfalme waliona visu, mapanga na sarafu.

**F. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika hali timilifu.**

***Mfano:*** *Mama anamuamsha Mboni.*

*<u>Mama amemuamsha Mboni</u>.*

1. Wanafunzi wanapiga picha za ukumbusho.
2. Mboni anawasimulia wenzake ndoto aliyoiota.
3. Baba aliniambia nizime taa.
4. Ninasoma kitabu cha hadithi.
5. Mama anatayarisha kifunguakinywa.
6. Wanafunzi watatembelea mapango ya Amboni.
7. Ndoto yangu ilitabiri ziara yetu.
8. Tutatembelea kaburi la Rais wa kwanza wa Zanzibar.



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 84 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**G. Tumia baadhi ya herufi za maneno yafuatayo kuunda maneno mapya yasiyopungua manne (4).**

***Mfano:*** *pakia - paka, kaa, pika, kipa.*

1. tangawizi
2. mfuasi
3. changamoto
4. makumbusho
5. simulia
6. takasa
7. maua
8. sufuria
9. mtumwa
10. umiza

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 85 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Moja

## Kuandika hadithi

Sura hii inahusu utungaji wa hadithi. Katika sura hii utasimulia na kusoma hadithi. Vilevile, utaweza kuandika hadithi kwa mtiririko sahihi wa matukio. Pia, utaweza kutumia alama za uandishi kwa usahihi.

**Fikiri**

1. Umeshawahi kusoma au kusimuliwa hadithi?
2. Hadithi hizo zilihusu nini?
3. Hadithi zipi zilikuvutia?
4. Kwa nini zilikuvutia?

## Ufahamu

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Kabula na Bahati

Hapo zamani za kale palikuwa na kijana mmoja aitwaye Bahati. Bahati alikuwa mtoto yatima. Wazazi wake walifariki akiwa mdogo. Baada ya wazazi wake kufariki, alikwenda kuishi kwa shangazi yake. Shangazi alikuwa na mtoto wa kike aitwaye Kabula. Mama yake Kabula hakumpenda Bahati. Alimpa kazi nyingi kila wakati. Kabula alipewa kazi nyepesi lakini kazi ngumu alipewa Bahati. Kabula aligundua hayo na aliumia sana. Kila wakati mama yake Kabula **alimkalia kitako** Bahati bila sababu yoyote. Bahati alijitahidi kuwa mtoto mwema lakini haikusaidia.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Siku moja mchana mama yake Kabula alimtuma Bahati kwenda porini kutafuta kuni peke yake. Bahati alikubali. Kabula alisikia maneno ya mama yake na kumuomba afuatane na Bahati. Mama yake alimkataza, akamwambia akachote maji. Kabula alikubali kwa **shingo upande.**



Bahati alichukua panga na kamba ya kufungia kuni akaondoka. Huko porini, kulikuwa na miti mikubwa na mirefu sana. Ilikuwa ni wakati wa masika, hivyo miti haikuwa imekauka. Alilazimika kwenda mbele zaidi. Alipouona mti mkavu alifurahi sana. Akasogea akaanza kuukata. Alifanikiwa kupata kuni za kutosha.

Bahati alijitwisha mzigo wa kuni na kuanza kurudi nyumbani. Maskini Bahati! Alisahau njia aliyopita awali. Alijaribu kuzunguka porini akiwa na mzigo wake kichwani, lakini hakuikumbuka njia. Hatimaye alichoka na kuamua kukaa chini ya mti huku akilia.

Ilipofika jioni, Kabula alimuuliza mama yake, “Mama mbona Bahati harudi? Mimi nataka kumfuata.” Mama alimwambia Kabula, “Usiende giza limeingia. Porini kuna wanyama wakali.” Kabula akasema “Mama, ina maana Bahati yeye haogopi wanyama wakali?” Mama yake alimjibu huku akifoka, “Sijui kumetokea nini, hajarudi mpaka muda huu! Fikiria tangu



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 87 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

aondoke mchana hadi sasa hajaleta kuni, siyo uvivu huo? Mkaa usingekuwepo ina maana leo tusingepika chakula?"

Kabula hakuridhika na majibu ya mama yake. Aliamua kutoka na kumfuata jirani yao aitwaye mama Huruma. Alipofika alimweleza yaliyotokea. Mama Huruma alisikitika sana. Alimweleza mume wake. Waliondoka na Kabula kwenda kumtafuta Bahati. Walipofika porini walimwita, "Bahati! Bahati!" Walizidi kusonga mbele huku wakimulika tochi. Bahati alisikia sauti kwa mbali ikimwita. Alisimama na kupaza sauti akisema, "Nipo huku!" Baba Huruma akamuuliza mkewe, "Umesikia sauti?" Mara Bahati akaitika tena, "Niko huku!" Walielekea upande ilikotoka sauti na kumkuta Bahati akiwa amechoka.

Kabula alipomwona Bahati alilia kwa furaha na kumkumbatia. Mama Huruma alisema, "Pole sana mwanangu." Huku akimshika mkono. Baba Huruma alichukua mzigo wa kuni kisha wote waliondoka kuelekea nyumbani. Walipofika nyumbani, mama Kabula alishangaa kumuona baba na mama Huruma wakiwa na Kabula na Bahati. Mama Kabula alipokea kuni na kuwakaribisha. Kuanzia siku hiyo shangazi alibadilika na kuonesha upendo kwa Bahati. Bahati aliishi kwa furaha na kuendelea kusoma kwa bidii.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Hadithi uliyoisoma inahusu nini?
2. Mama yake Kabula alikuwa na tabia gani?
3. Katika hadithi hii tabia ya nani imekuvutia? Kwa nini?
4. Mama yake Kabula angekuwa mama yako ungemshauri nini?
5. Kwa nini Kabula aliamua kwenda kumweleza Mama Huruma kuhusu Bahati?
6. Hadithi uliyoisoma ni ya kufurahisha au ya kusikitisha? Kwa nini?
7. Hadithi hii inatufundisha nini?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 88 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi moja kwa kila neno.**

1. porini
2. yatima
3. ghafla
4. jirani
5. mpole
6. twika

## Zoezi la 3 Nahau

**Oanisha nahau na maana zake.**

| Nahau | Maana |
|---|---|
| i. kalia kitako | (a) sikitika |
| ii. shika tama | (b) sijiwezi |
| iii. shingo upande | (c) sengenya |
| iv. tia moyo | (d) kutokuridhika |
| v. sina hali | (e) kalia kiti |
| | (f) kumpa mtu matumaini |

## Zoezi la 4 Mazoezi ya lugha

**A. Andika NDIYO au HAPANA.**

1. Hadithi ni masimulizi ya kubuni. ____________
2. Hadithi huburudisha na huelimisha. ____________
3. Ukiandika hadithi si lazima kuweka alama za uandishi. ____________
4. Hadithi inaweza kusomwa au kusimuliwa. ____________
5. Hadithi huwekwa kichwa cha habari. ____________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Badili majina yafuatayo kuwa vitendo.**

***Mfano:*** *onesho – onesha*
*upendo – penda*

1. somo ____________
2. mwandiko ____________
3. mchezo ____________
4. mchoro ____________
5. maelezo ____________

**C. Badili sentensi zifuatazo katika hali ya mazoea.**

***Mfano:*** *Wanafunzi wanakwenda shuleni kila siku.*
*Wanafunzi huenda shuleni kila siku.*

1. Wanyama wanakimbia mbugani.
2. Nyuki anatafuta chakula kwa ajili ya kutengeneza asali.
3. Wanafunzi wanajisomea baada ya masomo.
4. Garimoshi linasafiri kutoka Kigoma hadi Dar es Salaam.
5. Watoto wachanga wanalia wanapotaka kulala.

**D. Panga sentensi zifuatazo katika mfuatano sahihi wa matukio.**

1. Mama yake Kabula hakumpenda Bahati.
2. Hapo zamani za kale waliishi vijana wawili waliokuwa marafiki.
3. Bahati alichukua panga kuelekea porini.
4. Siku moja mama yake Kabula alimtuma Bahati kwenda porini kutafuta kuni.
5. Wazazi wake Bahati walifariki akiwa mdogo.
6. Ndugu hao walikuwa Kabula na Bahati.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Andika kinyume cha maneno haya.**

1. nje ________
2. shuka ________
3. wahi ________
4. meza ________
5. kata ________
6. nenda ________
7. lia ________
8. ingiza ________
9. rafiki ________
10. legeza ________

**F. Pigia mstari maneno ambayo ni vitendo katika sentensi zifuatazo:**

***Mfano:*** *Bahati alikwenda porini.*

1. Mama Huruma aliandaa chakula cha familia.
2. Baba alibeba panga na tochi.
3. Chatu alimeza mnyama.
4. Kabula na Bahati wanacheza pamoja.
5. Njela alichota maji bombani.

**G. Ondoa silabi moja tu katika maneno yafuatayo ili kuunda neno jipya.**

***Mfano:*** *kondoo – ndoo*

1. mkasi
2. funguo
3. kisasi
4. kabati
5. miwani
6. hodari
7. duwaa
8. usiku
9. mendea
10. mchezo

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**H. Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha andika kwa usahihi kwa kuzingatia alama za uandishi.**

siku moja njelani alisafiri kwenda mjini aliposhuka kwenye basi alisimama kwa muda akitazama huku na huko hakujua aelekee wapi kwa kuwa alikuwa mgeni ghafla alisikia sauti ikimwita njelani njelani alipogeuka alimwona sela njelani alifurahi sana akamwambia afadhali tumekutana naomba unipeleke madukani nikanunue viatu

## Zoezi la 5 Utungaji

**Wasimulie wenzako hadithi yoyote unayoifahamu kisha waambie wataje mafunzo yanayotokana na hadithi hiyo.**

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 92 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Mbili

## Mahali tulipo

Katika sura hii utajifunza kuonesha mahali watu na vitu vilipo. Utaweza kuandika sentensi zenye kuonesha mahali watu walipo na mahali vitu vilipo.

**Fikiri**

Umewahi kupanda juu ya mti? Kwa nini?

## Ufahamu

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Jinsi nilivyonusurika

Siku moja nilikuwa naelekea kijijini Mkoka kwa shangazi. Nilipogeuka nyuma nilishtuka sana kumwona mbwamwitu nyuma yangu. Nikapanda juu ya mti kujiokoa.

**Nilipotupa jicho** pembeni mwa mti niliona kibanda chakavu. **Mbwamwitu** alipita taratibu akakaa karibu na kibanda hicho. Nilipanda juu ya mti ili kujiokoa. Lakini jitihada zangu **hazikuzaa matunda**. Nikiwa juu ya mti nilimuona nyoka akiwa pembeni yangu. Niliogopa sana, nikashuka chini ya mti kwa kasi.

Nilijaribu kupiga kelele kwa nguvu lakini sauti haikutoka. Nilijirusha chini na kuanza **kupiga mbio** kuelekea mtoni. Ng'ambo ya mto kulikuwa na nyumba chache.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 93 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Nilianza kuelekea ziliko nyumba hizo. Nilipotaka kuvuka mto nilisikia sauti kama ya mtu anayeogelea. Kumbe alikuwa mamba mkubwa, nikaogopa kuvuka. Nilisimama kando ya mto huku nikiendelea **kupiga yowe**.

Watu walitoka ndani ya nyumba wakanikuta **macho yamenitoka**. Kabla ya kutoa msaada waliniambia "Baraka! Rudi nyuma kaa mbali na mto." Walimpiga mamba kwa mawe, fimbo na mikuki lakini alikimbia na kuzama. Hata hivyo, mamba alikuwa amekwisha jeruhiwa. Siku iliyofuata, wavuvi walimuona akielea pembeni mwa mto akiwa amekufa.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Msimuliaji wa habari hii anaitwa nani?
2. Kwa nini msimuliaji alipanda juu ya mti?
3. Msimuliaji aliposhuka chini alifanya nini?
4. Mnyama gani alikaa karibu na kibanda chakavu?



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 94 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Msimuliaji aliona nini ng'ambo ya mto alipokuwa anataka kuvuka?
6. Kama wewe ungekuwa msimuliaji ungefanya nini?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. kibanda
2. kasi
3. jeruhi
4. kando
5. chakavu
6. okoa

## Zoezi la 3 Miundo

**Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.**

1. …………… juu ya …………
2. ……………chini ya ……………………
3. ……………pembezoni mwa ……………
4. …………… karibu ya ………………………
5. …………… kando ya ……………………
6. …………… ndani ya………………

## Zoezi la 4 Nahau

**Andika maana za nahau zifuatazo kama zilivyotumika kwenye hadithi.**

1. piga yowe
2. zaa matunda
3. tupa jicho
4. toa macho
5. piga mbio

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5 Zoezi la lugha

**Chagua jibu sahihi kwenye mabano ili kukamilisha sentensi zifuatazo:**

1. Kijiko kipo ____________ kikombe. (ndani ya, mbele)
2. Tunapopika sufuria huwekwa ____________ jiko. (juu ya, kando)
3. Ndege ametua __________ mti. (ndani ya, juu ya)
4. Nyumba ipo ____________ ya mto. (juu, kando)
5. Baraka anapanda _____________ ya mti. (chini, juu)
6. Kiboko anaishi ____________ya maji. (mbele, ndani)
7. Mafuta yamo________ya chupa. (juu, ndani)

## Zoezi la 6 Vitendawili

**Tegua vitendawili vifuatavyo:**

1. Utupacho wewe kwake ni dhahabu.
2. Kuku wangu katagia mibani.
3. Watoto wa tajiri wa nguo hulala na kutembea uchi.
4. Viti vyote nimekalia isipokuwa hicho.
5. Wana wa mfalme ni wepesi sana kujificha.
6. Mama hachoki kunibeba.
7. Shamba langu ni kubwa lakini mazao ni kidogo sana.
8. Zulia la Mungu.
9. Jinamizi laniita lakini silioni.
10. Nina chemchemi isiyokauka.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 96 7/23/21 2:59 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 7 Utungaji

**Angalia picha kisha tunga sentensi moja kwa kila picha.**

1. 

2. 

3. 

4. 

5. 

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 97 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tatu

## Dawa za kulevya

Katika sura hii utasoma shairi linalohusu "Dawa za kulevya." Vilevile, utaweza kujifunza madhara ya dawa za kulevya. Pia, utaweza kuandika habari fupi kuhusu dawa hizo.

**Fikiri**

1. Unaelewa nini juu ya dawa za kulevya?
2. Dawa za kulevya zina madhara gani?

## Ufahamu

Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali.

### Dawa za kulevya ni hatari

1. *La mgambo likilia, ujue kunalo jambo,*
   *Ndugu kwenye familia, hutakiwi kwenda kombo,*
   *Vijana wazee pia, lisikie hili jambo,*
   *Ni hatari kutumia, dawa hizi za kulevya.*

2. *Dawa tukizitumia, haifai asilani,*
   *Jamii inakataa, hata vitabu vya dini,*
   *Madhara yameshajaa, kila pembe duniani,*
   *Ni hatari kutumia, dawa hizi za kulevya.*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 98 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. *Sindano mnachangia, mkijidunga mwilini,*
*Kutwa kucha mwasinzia, nyumbani hata njiani,*
*Jamii yawakataa, mpitapo mitaani,*
*Ni hatari kutumia, dawa hizi za kulevya.*

4. *Pombe kali mwajinywea, mnashinda vilabuni,*
*Masomo mnakimbia, hamwendi madarasani,*
*Wasichana mwaishia, kwa mimba za utotoni,*
*Ni hatari kutumia, dawa hizi za kulevya.*

5. *Mwatumia kila mara, vinywaji vyenye kileo,*
*Pombe na dawa si bora, kila iitwapo leo,*
*Mtayapata madhara, yanayoacha vilio,*
*Ni hatari kutumia, dawa hizi za kulevya.*

6. *Bangi, unga na kokeni, na nyingine kama hizo,*
*Mnajificha porini, mkila bila vikwazo,*
*Hizo zitawaueni, ni mbaya sio mchezo,*
*Ni hatari kutumia, dawa hizi za kulevya.*

7. *Jamii tubadilike, mbele tupate sogea,*
*Changamoto tuepuke, ya vileo kutumia,*
*Na tuzipige mateke, tabia zisizofaa,*
*Ni hatari kutumia, dawa hizi za kulevya.*

8. *Mtarukwa na akili, kupoteza nguvu kazi,*
*Fanyeni yalo halali, mtaongeza ujuzi,*
*Katika kila shughuli, mzingatie makuzi,*
*Ni hatari kutumia, dawa hizi za kulevya.*

9. *Wazazi muwe makini, ondosheni changamoto,*
*Fatilia kwa makini, nyendo za wako watoto,*
*Shuleni hata nyumbani, hakuna njia mkato,*
*Ni hatari kutumia, dawa hizi za kulevya.*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 99 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

10. *Taifa linawataka, vijana kubadilika,*
*Akina dada na kaka, na wazee mwahusika,*
*Ujumbe umeshafika, dawa tutaziepuka,*
*Ni hatari kutumia, dawa hizi za kulevya.*

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. "La mgambo likilia, ujue kunalo jambo." Maana yake nini?
2. Mwandishi ana maana gani anaposema, "Tuzipige mateke tabia zisizofaa."
3. Mtumiaji wa dawa za kulevya hupata madhara gani?
4. Katika shairi hili wazazi wamekumbushwa kufanya nini?
5. Unafikiri nini kifanyike ili kuepuka matumizi ya dawa za kulevya?
6. Utamshauri nini mtu anayetumia dawa za kulevya?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. familia
2. dawa
3. madhara
4. asilani
5. makini
6. kinywaji

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 100 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Mazoezi ya lugha

**A. Oanisha maneno ya sehemu A na maana zake katika sehemu B.**

***Mfano:*** *madhara - uharibifu au athari mbaya.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| i. kando | (a) kamwe |
| ii. asilani | (b) hali ya kulewa kutokana na matumizi ya vitu vinavyolewesha kama vile pombe na dawa za kulevya |
| iii. madhara | (c) tukio la hatari lisababishalo taabu na maafa |
| iv. kilabuni | (d) mahali palipo jirani na mahali pengine |
| v. janga | (e) kitu kinachofanana na kingine |
| vi. ulevi | (f) uharibifu au athari mbaya |
| | (g) sehemu inayouzwa pombe za kienyeji |

**B. Andika wingi wa maneno yafuatayo:**

| Umoja | wingi |
|---|---|
| 1. janga | ____________ |
| 2. taifa | ____________ |
| 3. sindano | ____________ |
| 4. kilabu | ____________ |
| 5. dawa | ____________ |
| 6. jamii | ____________ |
| 7. changamoto | ____________ |

**C. Andika maneno yafuatayo kuonesha mahali.**

***Mfano:*** *shule* *shuleni*

1. nyumba ____________
2. darasa ____________



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 101 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. njia ____________
4. msitu ____________
5. hospitali ____________
6. uwanja ____________

**D. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

1. hasara ___________
2. huzuni ___________
3. lia ___________
4. funika ___________
5. mbele ___________
6. ondoa ___________
7. kijana ___________

**E. Unda neno jipya kwa kudondosha silabi au herufi.**

***Mfano:*** *(a) taifa – tai*

*(b) kulevya – kule*

1. katika ___________
2. kijana ___________
3. dunia ___________
4. kifani ___________
5. vitabu ___________
6. kilevi ___________

**F. Andika KWELI au SI KWELI.**

1. Dawa za kulevya hupoteza nguvu kazi ya taifa. ___________
2. Mtu anayetumia dawa za kulevya hawezi kupata UKIMWI. ___________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Kutumia dawa za kulevya ni kuvunja sheria ya nchi. __________

4. Mtu anayetumia dawa za kulevya hapaswi kuigwa na jamii. __________

5. Kama rafiki yako akitumia dawa za kulevya mshauri aache. __________

6. Mtu anayetumia dawa za kulevya hupata vishawishi vya kutenda maovu. __________

## G. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuchagua jibu sahihi.

1. Kushirikiana............ kunachangia kueneza UKIMWI. (maji, mavazi, malazi, sindano)

2. ................ wanapaswa kuepuka mimba za utotoni. (wavulana, bibi, wazee, wasichana)

3. Utumiaji wa dawa za kulevya husababisha ................... kiafya. (upendo, vita, madhara, amani)

4. Taifa linataka .................... kujiepusha na matumizi ya dawa za kulevya.

   (watu wote, baadhi ya watu, watu wengi, watu binafsi)

5. Miongoni mwa dawa za kulevya ni kama .............. (mirungi na bangi, moshi na bangi, moshi na mirungi)

## H. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wakati ujao.

1. Mimi nimeepuka kutumia dawa za kulevya.

2. Wasichana wanafundishwa madhara ya mimba za utotoni.

3. Jamii imebadilika kutokana na vita dhidi ya dawa za kulevya.



FOR ONLINE USE ONLY

Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 103 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Wananchi wamefurahi kukomeshwa kwa matumizi ya dawa za kulevya.
5. Kuzuiwa kwa dawa za kulevya kumepunguza wizi.

## Zoezi la 4 Utungaji

**Andika habari yenye maneno sabini (70) kuhusu madhara ya dawa za kulevya.**

Maswali yafuatayo yatakuongoza:

1. Unaelewa nini kuhusu dawa za kulevya?
2. Dawa za kulevya zina madhara gani?
3. Jamii inapaswa kufanya nini kuhusu dawa za kulevya?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 104 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Nne

## Kuchemsha chai

Sura hii inahusu utungaji. Utajifunza jinsi ya kufuata maelekezo na hatua sahihi katika kutenda jambo kama vile mapishi ya chai. Utaweza kuandika utungaji unaohusu jambo linalofanyika hatua kwa hatua.

**Fikiri**

1. Chai ni kinywaji cha aina gani?
2. Unafikiri chai hunywewa muda gani? Kwa nini?

## Ufahamu

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Kuchemsha chai

Mwalimu Zena ni mwalimu wa somo la upishi.

Kipindi kilichopita mwalimu alituambia tukusanye vifaa mbalimbali kwa ajili ya kuchemsha chai.



Kila mwanafunzi alikuja na vitu alivyoagizwa.

Wengine walileta majani ya chai, tangawizi na baadhi walileta sukari. Kabla ya kuanza kuchemsha chai mwalimu aliuliza maswali.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mwalimu:** Ni muda gani unakunywa chai?

**Sada:** Asubuhi mwalimu.

**Mwalimu:** Ni chai gani unayoipenda?

**Kapi:** Chai ya rangi.

**Sofia:** Mimi napenda chai ya maziwa.

**Mwalimu:** Asanteni sana. Leo tutajifunza jinsi ya kuchemsha chai ya rangi. Ili kupata chai ya rangi tutachanganya viungo gani?

**Mashaka:** Majani ya chai, maji na sukari

**Mwalimu:** Ni sawa kabisa. Pia baadhi ya watu hupenda kuweka iliki na mdalasini katika chai ili kuweka harufu nzuri. Mmeelewa?

**Wanafunzi:** Ndiyo mwalimu.

**Mwalimu:** Tutajifunza kuchemsha chai ya rangi kwa kutumia jiko la gesi. Andaa vifaa vyote vinavyohitajika katika upishi wa chai. Weka sufuria yenye maji kwenye jiko lililowashwa. Weka tangawizi na viungo vingine kama utapenda. Maji yanapokaribia kuchemka weka majani ya chai na uiache ichemke kwa muda. Epua, chai yetu iko tayari kwa kunywewa.

Mwalimu alisema kila mwanafunzi ataweka sukari mwenyewe. Baada ya hapo sote tulikunywa chai.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Mwalimu Zena alitufundisha nini?
2. Wanafunzi walitakiwa kuleta vitu gani kwa ajili ya upishi wa chai?
3. Hatua zipi zilifuatwa na wanafunzi wakati wa kuchemsha chai?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Kwa nini walitumia jiko la gesi badala ya jiko la mkaa au kuni?
5. Kwa nini mwalimu alisema kila mtu aweke sukari mwenyewe?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tumia maneno yafuatayo kutunga sentensi mbili kwa kila neno.**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **epua** | **chemka** | **upishi** | **vifaa** | **viungo** |

## Zoezi la 3 Mazoezi ya lugha

**A. Oanisha maneno ya sehemu A na B ili kukamilisha sentensi.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| i. Mwalimu Zena | (a) jiko la gesi |
| ii. hatua ya kuchemsha chai | (b) asubuhi |
| iii. muda wa kawaida wa kunywa chai | (c) maji na jiko |
| iv. majani ya chai, maji na sukari | (d) mahitaji ya upishi wa chai ya rangi |
| v. hutumika kupikia badala ya jiko la kuni au la mkaa | (e) anafundisha somo la upishi |
| | (f) chemka |
| | (g) majani ya chai |
| | (h) kuweka sufuria yenye maji kwenye jiko linalowaka |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 107 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi kwa kuzingatia alama za uandishi.**

1. maziwa yaliyoganda hayafai kupikia chai
2. Tanzania inazalisha mazao mbalimbali kwa mfano chai kahawa na kakao
3. viungo vya chai ni tangawizi mchaichai mdalasini na iliki
4. unapopika chai kwanza unawasha jiko unachemsha maji kisha unaweka viungo
5. mwalimu zena alitufundisha kupika chai ya rangi

**C. Panga maneno yafuatayo ili kupata sentensi zenye maana.**

***Mfano:*** *Wanafunzi chai shuleni walichemsha.*

*<u>Wanafunzi walichemsha chai shuleni.</u>*

1. Upishi mwalimu wa Zena ni.
2. Chai tunakunywa asubuhi sote.
3. Rangi ya sana chai tamu ni.
4. Maziwa hupenda chai ya watu wengi.
5. Chai yao walikunywa walimu ofisini.

**D. Andika sentensi zifuatazo katika wakati uliopita.**

*Mfano: Amina anaimba wimbo mzuri.*

*Amina <u>aliimba</u> wimbo mzuri.*

1. Jerome anauza maziwa.
2. Wanafunzi wamewahi shuleni.
3. Sofia anafua nguo na kupika chakula.
4. Babu atawasimulia wajukuu zake hadithi.
5. Mwanahawa anauza mahindi gulioni.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 108 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Majangili wamekamatwa wakiwinda wanyama.
7. Fundi Juma atashona sare za harusi.
8. Wavuvi wamevua samaki wengi.

**E. Tunga sentensi sita (6) sahihi kutoka katika jedwali lifuatalo:**

| | | |
|---|---|---|
| Nilijitahidi<br>Nilizingatia masomo<br>Alikimbia sana | akawa<br>nikawa | wa kwanza<br>mshindi<br>mwanafunzi bora darasani |

**F. Jaza nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi zifuatazo:**

1. Mgeni alipobisha ......................... alikaribishwa.
2. Alipokuwa na ......................... aliomba maji ya kunywa.
3. Alitumia ......................... kunyoosha nguo zake.
4. Timu yetu imeshinda kwa ......................... mengi
5. Bibi alifinyanga ......................... vizuri.

**G. Ongeza silabi moja mbele au nyuma kuunda maneno mapya.**

***Mfano:*** *nepa - nenepa*

1. kata ____________
2. zizi ____________
3. meza ____________
4. kaa ____________
5. taa ____________
6. kanda ____________
7. chota ____________
8. kasi ____________
9. paka ____________
10. uza ____________

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 109 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4 Utungaji

**Andika habari fupi isiyozidi maneno sabini (70) kwa kutumia picha zifuatazo:**

Andika kichwa cha habari juu ya habari yako.

1.



2.



3.



4.



FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 110 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5.



**Zoezi la 5 Kazi ya kufanya**

**Andika hatua za kupika viazi vitamu kwa kuzingatia:**

1. Matayarisho: Maandalizi ya vitu na vifaa utakavyotumia kupikia.
2. Jinsi ya kupika: Hatua ya kwanza hadi hatua ya mwisho.
3. Mwisho wa upishi na sehemu ya kuweka kwa ajili ya kuliwa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tano

## Kuandika barua

Katika sura hii utajifunza jinsi ya kuandika barua ya kirafiki. Utaweza kueleza muundo wa barua ya kirafiki na kuandika barua ya kirafiki kwa usahihi.

**Fikiri**

1. Je, umewahi kuandika barua?
2. Ulimwandikia nani?
3. Barua hiyo ilikuwa inahusu nini?
4. Ni vipengele vipi vilitumika katika barua hiyo?

## Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Ziara kiwandani Mtibwa

Kabula ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kabingo. Anasoma Darasa la Nne. Ni mwanafunzi anayejitahidi kusoma kwa bidii na anafanya vizuri katika masomo yake. Wazazi wake wanafurahia sana maendeleo yake.

Siku moja mwalimu wa Kiswahili alipoingia darasani, aliwafundisha kuhusu mimea mbalimbali iliyopo katika mazingira yao. Wanafunzi wengi walitaja aina za mimea wanayoifahamu. Miongoni mwa mimea iliyotajwa ni miwa. Kabula alimwambia mwalimu kuwa hajawahi kuona mashamba ya miwa. Mwalimu aliwaeleza kuwa mwezi ujao ataandaa ziara ya kwenda Mtibwa



FOR ONLINE USE ONLY

Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 112 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ambako kuna mashamba makubwa ya miwa. Pia aliwaambia kwamba tunapata sukari kutokana na miwa.

Kabula alifurahi kusikia kuwa watakuwa na safari ya kwenda Mtibwa. Hivyo alimwandikia baba yake barua kumuomba nauli na fedha za kujikimu wakati wa safari. Barua hiyo ilikuwa kama ifuatavyo:

Shule ya Msingi Kabingo,
S.L.P. 44,
Kigoma.
12.3.2018.

Mpendwa baba, shikamoo.

Ni matumaini yangu kuwa wote hapo nyumbani ni buheri wa afya. Kwa upande wangu mimi sijambo na ninaendelea vizuri na masomo.

Madhumuni ya barua hii ni kukujulisha kuwa, shule yetu inatarajia kufanya ziara. Wanafunzi wa Darasa la Nne tutatembelea Kiwanda cha Sukari Mtibwa. Kiwanda hicho kipo mkoa wa Morogoro wilaya ya Mvomero. Ninaomba unitumie shilingi elfu hamsini na tano kwa ajili ya kujikimu na kulipia nauli. Mara tutakoporudi, tutafanya mitihani ya kumaliza muhula. Ninajitahidi kusoma kwa bidii ili niweze kufaulu vizuri. Pia, nitadumisha nidhamu muda wote na sitakengeuka. Ninatamani kufikia ndoto yangu ya kuwa daktari.

Ninakutakia kazi njema. Wasalimie wadogo wangu wote.

Mimi mwanao,
Kabula

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Je, barua ya kirafiki ina umuhimu gani?
2. Kwa nini Kabula alimwandikia baba yake barua?
3. Je, unafikiri Kabula katika familia yao ni mtoto wa ngapi?
4. Je, unafikiri Kabula ana tabia gani?
5. Je, ungependa kuwa na tabia kama ya Kabula? Kwa nini?

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. ziara 2. kujikimu 3. bidii 4. kukengeuka 5. ndoto

## Zoezi la 3 Mazoezi ya lugha

**A. Chunguza miundo hii inayotumika katika barua za kirafiki kisha jibu maswali.**

1. Baba mpendwa, au shikamoo, au Mpendwa baba, au salaamu sana .............
2. Madhumuni ya barua hii ni …......... au lengo la barua hii ni.........
3. Napenda kukuarifu kuwa ............
4. Upatapo barua hii ......................
5. Wasalaam mimi .......................
6. Ndimi mwanao ...................... ...

**Maswali**

(a) Je, umewahi kutumia miundo hii katika barua uliyowahi kuandika?

(b) Je, ni vipengele gani vingine ambavyo havikutajwa vinavyokamilisha muundo wa barua ya kirafiki?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 114 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B.** **Angalia vipengele vya muundo wa barua ya kirafiki katika jedwali. Weka vipengele hivyo katika mpangilio sahihi.**

| Vipengele vya muundo wa barua | Nafasi katika muundo |
|---|---|
| i. Jina na saini ya mwandishi | ____________ |
| ii. Mwisho wa barua | ____________ |
| iii. Utangulizi wa barua | ____________ |
| iv. Salamu ya awali | ____________ |
| v. Anuani ya mwandishi | ____________ |
| vi. Barua yenyewe | ____________ |
| vii. Tarehe | ____________ |

**C.** **Chunguza muundo huu wa barua ya kirafiki, kisha jaza visanduku ulivyopewa:**

1.

2.

3.

4.

5.

6.

7.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 115 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Andika KWELI au SI KWELI kuonesha kukubali au kukanusha wazo lililotolewa.**

1. Barua za kirafiki huandikwa kwa familia au rafiki tu.

   _______________

2. Anuani ya barua ya kirafiki haihitajiki kwani jina la anayeandika linatosha. _______________
3. Barua za kirafiki hutoa taarifa za familia, kijamii na kumpa pole rafiki. _______________
4. Barua ya kirafiki ni njia mojawapo ya kuwasiliana na rafiki, jamaa na familia. _______________
5. Mwisho wa barua ya kirafiki una sehemu zaidi ya sita.

   _______________

**E. Ufuatao ni muundo wa barua ya kirafiki na taarifa zake muhimu. Oanisha sehemu ya muundo katika sehemu 'A' na sehemu 'B' ili kuleta maana kamili.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| i. Barua yenyewe .............. | (a) Madhumuni au lengo la barua hii ni ................. |
| ii. Utangulizi wa barua .............. | (b) Ni matumaini yangu wote ............... |
| iii. Mwisho wa barua .............. | (c) Mpendwa baba, shikamoo. ......... |
| iv. Maamkizi ya awali .............. | (d) Ndimi/mimi mwanao / wasalam ............ |
| v. Anuani ya mwandishi ............. | (e) Bakari Kishingo ............. (saini) |
| vi. Jina na saini ya aliyeandika barua .............. | (f) 1/5/2018 |
| vii. Tarehe .............. | (g) S.L.P. 280, Njombe. |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 116 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**F. Eleza kinyume cha maneno uliyopewa.**

1. mwisho wa barua ____________________
2. mbichi ____________________
3. adui ____________________
4. mtiifu ____________________
5. mbali ____________________
6. bidii ____________________
7. kukubali ____________________
8. kifunguamimba ____________________
9. tamu ____________________
10. huzuni ____________________

## Zoezi la 4 Utungaji

**Andika barua kwa dada yako ukimuarifu kuwa tarehe ........ (Andika terehe ya likizo yako fupi) mtafunga shule. Hivyo unaomba hela ya nauli na matumizi ya njiani. Jina lako liwe Maua Imani na la dada yako liwe Sara.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Sita

## Kuandika hadithi fupi kwa kutumia majina ya ndege

Katika sura hii utasoma hadithi inayohusu ndege. Utaweza kutambua aina mbalimbali za ndege na majina yao. Pia, utaweza kuandika hadithi fupi kwa kutumia majina hayo.

### Fikiri

1. **Chunguza ndege wafuatao, kisha eleza:**

    (a) Tabia zao

    (b) Maumbo yao

    (c) Rangi zao



2. **Jadiliana na mwenzako**

    Kwa nini kunguru anaweza kuruka umbali mrefu kuliko bata?



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 118 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ufahamu

*Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Kunguru na bata

Hapo zamani za kale kunguru na bata walikuwa marafiki. Waliishi msituni wakitafuta chakula pamoja. Siku moja kunguru alimwambia bata, "Rafiki yangu nina jambo ambalo siwezi kulivumilia. Leo ni lazima nikueleze." Kunguru alizunguka huku na huko kwa hasira huku akibubujikwa na machozi. Alisema, "Bata umekuwa mvivu sana wa kutafuta chakula, unakula chakula changu kila siku."

Bata alihamaki na kusema, "Kwa nini unasema hivyo, nimekukosea nini?" Kunguru akajibu, "Kila siku mimi navuka mabonde na milima kwenda kutafuta chakula. Wewe umekaa tu, huoni kama unanidhulumu?" Bata aliposikia maneno hayo alilia kwa uchungu. "Haaa! Haaa! Haaa!" Akamwambia kunguru, "**Usilolijua ni sawa na usiku wa giza**, ipo siku utaujua ukweli."

Baada ya kusema hayo bata aliamua kumueleza kunguru kuhusu tofauti zao. Alianza kwa kusema, "Kunguru rafiki yangu, kumbuka kwamba viumbe tunatofautiana. Sisi sote ni ndege lakini kila mmoja ana sifa zake. Hebu tazama miguu yako na yangu, je, umeona tofauti? Hebu tazama umbo lako na langu, je tuko sawa? Hebu njoo uninyanyue ulinganishe uzito wako na wangu, je, tuko sawa? Ukijibu maswali haya utapata jibu kwa nini mimi siwezi kuruka juu zaidi kama wewe. Mimi pia naogopa kwenda mbali, ninaweza kupotea kwa kuwa sikumbuki njia ya kurudi." Kunguru aliposikia maneno ya bata aliumia sana moyoni. Alijutia maneno aliyomwambia bata.

Bata aliendelea kusema ,"**Msema kweli ni mpenzi wa Mungu**. Ngoja nikuambie ukweli. Nimeumia sana kwa maneno uliyoniambia. Kuanzia leo mimi na bata wenzangu tunaondoka kwenda kuishi na binadamu. Binadamu atatutunza vizuri,



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 119 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nasi tutamtagia mayai. Atatulisha nafaka, tutajenga miili yetu. Atatupatia matunda, tutajikinga na magonjwa. Vilevile, sisi tuna uwezo wa kuogelea katika mito, mabwawa na maziwa tukitafuta chakula. Kwa hiyo, kuanzia leo sisi tunaondoka." Kunguru aliwabembeleza bata wasiondoke kwa kulia, "Kwaaa! Kwaaa! Kwaaa." Bata hawakumwonea huruma, waliondoka msituni na kwenda kuishi na binadamu.

Bata walipofika kwa binadamu, walifurahi kuwakuta kuku, kanga, njiwa na kware. Maisha yakawa mazuri kwani binadamu aliwapa kila walichohitaji. Walimsimulia binadamu yaliyotokea kati yao na kunguru.

Kunguru walibaki msituni bila rafiki. Waliamua kwenda kuwatafuta ndege wengine. Walipokuwa njiani walikutana na mwewe, tai, korongo na bundi. Kunguru mmoja aliwaita, "Jamani njooni niwaambie yaliyotukuta." Wote wakatua katika mti mkubwa wa mkuyu.



Kunguru huku akiangua kicheko na kusema, "Ndugu zangu, tulikuwa na rafiki zetu bata lakini wametukimbia." Mwewe akadakia, "Wamekwenda wapi?" Kunguru akajibu, "Wamekwenda kuishi na binadamu." Tai alishangaa, "Hee!



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 120 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mmewafanya nini mbona bata ni wapole?" Kunguru akajibu, "Hatukuelewana kwa sababu ya uvivu wao. Hawataki kwenda mbali kutafuta chakula." Korongo akasema, "Kwani bata hawawezi kutafuta chakula?" Kunguru akajibu, "Ndiyo." Tai akasema, "Kama hawawezi mngekula wote chakula mlichotafuta ninyi." Kunguru wote wakaangua kicheko. "Haa! Haa! Haa! Haiwezekani."

Baadaye, kunguru aliwashauri wenzake waende kwa binadamu kutafuta chakula. Aliwambia ndege wengine waendelee kusubiri juu ya mti. Walipofika walimkuta bata yuko uwanjani na vifaranga wake sita. Binadamu alikuwa ndani ya nyumba. Kunguru walitua juu ya mti uliokuwa pembeni ya nyumba. Walipanga mbinu watakazotumia kuwakamata vifaranga wote wa bata.



Kunguru mmoja aliwaambia wenzake, "Tushuke wote kwa pamoja tumvamie bata, kabla ya kuchukua vifaranga." Baada ya kukubaliana kunguru walimvamia bata na wengine

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

walinyakua vifaranga. Tangu siku hiyo kunguru na bata ni maadui. Ndio maana bata daima huwalinda vifaranga wake kwa kuwatanguliza mbele wanapotembea na yeye hufuata nyuma.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Nani walikuwa marafiki katika hadithi uliyoisoma?
2. Kwa nini kunguru aliona kuwa anadhulumiwa na bata?
3. Kwa nini bata alilia kwa uchungu?
4. Kunguru alikuwa na tabia gani?
5. Unapenda tabia za nani kati ya kunguru na bata? Kwa nini?
6. Bata alifanya nini ili kuepusha ugomvi kati yake na kunguru?
7. Eleza mambo matatu uliyojifunza katika hadithi hii.
8. Simulia hadithi uliyoisoma kwa maneno yako mwenyewe.

## Zoezi la 2 Msamiati

**Chagua neno moja kutoka katika kisanduku kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **kale** | **tenga** | **hamaki** | **laumu** | **uchungu** | **nyanyasa** |

1. Shikwa na hasira kali na kufanya kitu bila kufikiri_______
2. Maumivu ayapatayo mtu kutokana na kuumia kiungo cha mwili au taarifa za kusikitisha ___________
3. Enzi za zamani__________
4. Kumnyima haki zake za msingi_________
5. Kumsema mtu kutokana na makosa yake_______
6. Weka kando_____________



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 122 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Methali na semi

**A. Eleza maana za methali na semi zifuatazo:**

1. Usilolijua ni sawa na usiku wa giza.
2. Leo ni leo, asemaye kesho mwongo.
3. Msema kweli ni mpenzi wa Mungu.
4. Mvumilivu, hula mbivu.
5. Dua la kuku, halimpati mwewe.
6. Uchungu wa mwana, aujuaye mzazi.

**B. Kamilisha methali zifuatazo kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kisha iandike katika kisanduku:**

1. Ndege mjanja,………………………...
   (a) hakamatwi na mtego
   (b) hunaswa kwenye tundu bovu
   (c) hukamatwa na ulimbo
   (d) huwa mwangalifu kwa kila jambo

2. Ndege asiyenaswa leo,……………………….
   (a) ni kitoweo cha kesho
   (b) hawezi kunaswa tena
   (c) harudi tena kwenye mtego
   (d) mtego wake ni mbovu

3. Kuku mgeni,………………………..
   (a) hakosi alama mguuni.
   (b) hakosi kamba mguuni
   (c) hakosi kushangaa
   (d) hupenda kuwika asubuhi



FOR ONLINE USE ONLY

Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 123 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Jogoo wa shamba, ..........
   (a) ana umbo kubwa
   (b) hawiki vizuri
   (c) hawiki mjini
   (d) haogopi watu

5. Ngojangoja, ................
   (a) utachelewa
   (b) hutamkuta
   (c) yaumiza matumbo
   (d) utamkuta

## Zoezi la 4 Miundo

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia miundo hii.**

| | | |
|---|---|---|
| .........walipokuwa......., | ....... huku na huko...., | |
| kila siku...., | ......lakini..., | ....... kwa sababu.... |

1. ............... kunguru huruka juu ya miti.
2. Alitazama ................ lakini hakuona mtu.
3. Bata alikwenda kuishi na binadamu ...........alishindwa kuishi na kunguru.
4. Kunguru alimfukuza bata ............. baadaye alisikitika.
5. Bata ..............kwa binadamu waliishi kwa amani.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 124 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

1. kubali ____________
2. rafiki ____________
3. sema ____________
4. lia ____________
5. nenda ____________
6. jenga ____________

**B. Tunga sentensi kumi kwa kutumia maneno yaliyomo katika jedwali lifuatalo:**

| | | |
|---|---|---|
| Baada ya<br>Kabla ya | kupanga mipango yao<br>kusikia maneno hayo<br>kukubaliana | kunguru wote waliruka<br>bata aliondoka<br>bata alilia kwa uchungu |

**C. Andika KWELI au SI KWELI katika sentensi zifuatazo:**

1. Ndege wote wana tabia zinazofanana. ________
2. Neno ndege lina maana zaidi ya moja. ________
3. Ndege wafugwao ni bata, njiwa na bundi. _______
4. Ndege wote hutaga mayai. _______
5. Ndege wote hula nafaka. _______

**D. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi kwa kuzingatia alama za uandishi.**

1. chiriku kunguru kuku na bata wote ni jamii ya ndege
2. katika mlima kilimanjaro kuna ndege wa kuvutia
3. mwalimu alisema ni muhimu kujifunza tabia za ndege
4. je kuna umuhimu wa kujifunza tabia za ndege
5. loo kunguru ana tabia mbaya
6. tai alishangaa mmewafanya nini bata

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 125 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E.** **Kutokana na chati ifuatayo, andika majina manne (4) ya ndege wanaofugwa.**

| | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | W | A | R | E | K | U | K | U | E | CH | U | E | T |
| U | T | U | A | B | A | T | A | M | Z | I | N | G | A |
| K | I | K | A | N | G | A | P | A | N | Z | I | B | I |
| B | K | O | R | O | N | G | O | M | W | E | W | E | V |
| N | J | I | W | A | CH | I | R | I | K | U | T | A | K |

## Zoezi la 6 Utungaji

**Andika hadithi fupi yenye maneno yasiyopungua sabini (70) kuhusu kuku na mwewe.**

Fuata mwongozo huu:

1. Hapo zamani za kale..........
2. Kuku na mwewe walifanya nini?
3. Tukio hilo lilitokea wapi?
4. Unapata fundisho gani kutokana na hadithi hiyo?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 126 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Saba

## Kujifunza mashairi

Katika sura hii utajifunza kuhusu mashairi. Utaeleza shairi ni nini, utasoma na kuimba shairi. Pia utafanya mazoezi na kujibu maswali kwa kuzingatia vina, mizani, mishororo na urari katika shairi.

**Fikiri**

1. Shairi huimbwa na nani?
2. Kitu gani kinachokufurahisha katika shairi?
3. Kwa nini kinakufurahisha?

Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali.

### Janga la UKIMWI

1. *Leo tumekusanyika, UKIMWI kuongelea,*
*Bara letu Afrika, Ulaya hadi Asia,*
*Hakuna usipofika, kote umeshasambaa,*
*Tusipokuwa makini, sote utatumaliza.*

2. *Kwanza nizitaje njia, jinsi unavyoenea,*
*Nyembe tunazochangia, si salama nakwambia,*
*Mswaki sio sawia, kama nyote tatumia,*
*Jamani tujihadhari, tusije tukapotea.*

3. *Vitu vyenye ncha kali, si vizuri kuchangia,*
*Vyaweza leta ajali, iwapo utakosea,*
*Sindano hospitali, hata mitaani pia,*
*Vitu vilivyovunjika, usipende sogelea.*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 127 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. *Mama kwenda kwa mtoto, wakati wa kuzaliwa,*
*Inaleta changamoto, wakati ukififikiwa,*
*Anapotoka mtoto, na asipoangaliwa,*
*Ni rahisi kwa mtoto, kupata maambukizi.*

5. *Ngono isiyo salama, nayo pia huchangia,*
*Wazee na kina mama, baba na vijana pia,*
*Ndoto zenu zitakoma, UKIMWI mkiugua,*
*Ni vizuri kujilinda, ili mbaki salama.*

6. *Sasa nakupa dalili, za UKIMWI kuzijua,*
*Kuharisha homa kali, na uzito kupungua,*
*Kudhoofu wako mwili, pasipo kutarajia,*
*Ukijilinda mapema, UKIMWI hautopata.*

7. *Kifua kikuu kwako, sana kitakusumbua,*
*Vidonda mdomo wako, chakula takichukia,*
*Vipele mwilini mwako, na ngozi itasinyaa,*
*Tujilinde na UKIMWI, ni maradhi hatarishi.*

8. *Ukiwa nao mwilini, usije kata tamaa,*
*Ishi kwa matumaini, lishe na dawa tumia,*
*Jitunze ujithamini, maisha kufurahia,*
*Usieneze zaidi, UKIMWI kwenye jamii.*

9. *Zinaonesha takwimu, watu wengi waugua,*
*Tena za kitaalamu, na zenye uhalisia,*
*Tahadhari ni muhimu, ili liweze pungua,*
*Janga hili la UKIMWI, taifa lisitoweke.*

10. *Wito kwa letu taifa, hili la Watanzania,*
*Tuyaepuke maafa, UKIMWI una fadhaa,*
*Tusambaze taarifa, kila kona kwa jamaa,*
*Taifa bila UKIMWI, hakika yawezekana.*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 128 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Shairi letu linahusu nini?
2. Je, shairi hili lina beti ngapi?
3. Je, kuna umuhimu gani kujifunza elimu ya UKIMWI?
4. Je, mishororo ya mwisho ya kila ubeti inafanana?
5. Ujumbe gani umepata kutokana na shairi hili?
6. Ubeti upi mtunzi wa shairi ameeleza mambo yafuatayo?
   (a) Kueneza taarifa za kuepukana na ugonjwa wa UKIMWI.
   (b) Kuwatia moyo wagonjwa waliopata maambukizi ya UKIMWI.
   (c) Ushauri wa kuzingatia lishe bora na kutumia dawa.
   (d) Maambukizi ya UKIMWI yatokanayo na ngono isiyo salama.
   (e) Tahadhari ya kutoeneza UKIMWI kwa jamii.
   (f) Uwezekano wa Watanzania kutopata maambukizi ya UKIMWI.

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. kinga
2. sambaa
3. maradhi
4. maambukizi
5. lishe
6. kusinyaa

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 129 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3 Mazoezi ya lugha

**A. Chagua jibu sahihi, kisha jaza nafasi iliyoachwa wazi.**

1. Mstari mmojawapo kwenye kila ubeti huitwa__________
   (a) mizani
   (b) urari
   (c) mshororo
   (d) kituo

2. Silabi zinazofanana katikati au mwishoni mwa mstari mmoja wa shairi huitwa__________
   (a) urari
   (b) pigo
   (c) mizani
   (d) vina

3. Idadi ya silabi katika mstari mmoja wa shairi unaitwa______
   (a) vina
   (b) mizani
   (c) mshororo
   (d) pigo

4. Aya ya shairi huitwa ___________
   (a) mizani
   (b) mshororo
   (c) ubeti
   (d) vina

5. Mstari wa mwisho katika ubeti wa shairi unaitwa______
   (a) kituo
   (b) mshororo
   (c) vina
   (d) ubeti

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 130 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Mshairi anatoa ujumbe gani katika ubeti wa tisa?________
   (a) Tusisambaze taarifa kila kona kwa jamaa.
   (b) Takwimu za kitaalamu zinaonesha watu wengi wanaugua.
   (c) Taifa bila UKIMWI hakika haiwezekani.
   (d) Watu wengi wajihadhari na UKIMWI.

7. Katika ubeti wa nane mshairi anatoa ushauri gani?_______
   (a) Kujilinda na UKIMWI.
   (b) Kutochangia mswaki.
   (c) Kuepukana na maafa.
   (d) Kutumia dawa na lishe bora.

## B. Andika NDIYO au HAPANA.

1. UKIMWI hauambukizwi kwa njia ya hewa. __________
2. Mtu anayeishi na Virusi vya UKIMWI utamtambua kwa kumuona. _________________
3. Kinga ni bora kuliko tiba. _______________________
4. Watoto wachanga hawaambukizwi Virusi vya UKIMWI. _________________
5. Tunashauriwa kutopima Virusi vya UKIMWI mara kwa mara. _____________________
6. Taifa hupoteza nguvu kazi kwa kuwa na wagonjwa wa UKIMWI. ___________

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 131 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Andika kwa ukamilifu maneno haya yaliyotumika katika shairi.**

***Mfano:*** *kata – kukata*

1. tumia
2. sogelea
3. leta
4. takichukia
5. pungua

**D. Oanisha maneno yaliyo katika sehemu A na sehemu B ili kuleta maana.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| i. dhoofu | (a) ukosefu wa kinga mwilini |
| ii. maradhi | (b) kitu kinachotumika kuponya ugonjwa |
| iii. sinyaa | (c) sayansi inayohusu ukusanyaji, uainishaji na tafsiri ya taarifa za idadi |
| iv. changamoto | (d) kushindwa kuwa na hali njema ya afya |
| v. UKIMWI | (e) maumivu na usumbufu wa kiafya anaoupata mgonjwa |
| vi. takwimu | (f) usambazaji wa ugonjwa kutoka kiumbe mmoja kwenda kwa mwingine |
| vii. tiba | (g) madhara makubwa mfano uharibifu wa mali na vifo |
| viii. maambukizi | (h) kuwa katika hali ya mapungufu |
| | (i) jambo linalomkabili mtu na analohitaji kulitatua |
| | (j) kukonda na kuishiwa na nguvu na kupungukiwa na afya |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 132 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## E. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:

| Neno | Kinyume |
|---|---|
| 1. dhoofu | ________ |
| 2. nzito | ________ |
| 3. kusanya | ________ |
| 4. pangua | ________ |
| 5. ndogo | ________ |
| 6. pata | ________ |
| 7. chukia | ________ |
| 8. ugonjwa | ________ |

## F. Andika neno lenye maana sawa na maneno yafuatayo:

***Mfano:*** *mtu - binadamu*

1. rika ____________
2. shida ____________
3. safi ____________
4. tunza ____________
5. ajuza ____________
6. tamati ____________
7. awali ____________
8. pipi ____________

## G. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno uliyopewa katika kisanduku.

| mkubwa | mdogo | kikubwa | kidogo |
|---|---|---|---|

***Mfano:*** *Kiatu kikubwa hakikumtosha.*
*Kiatu kidogo hakikumtosha.*

1. Kiti..............kilivunjika kabisa.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 133 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Msichana ...............aliwasaidia wenzake.
3. Kikosi ................ kilipambana.
4. Kiazi............kilipikwa asubuhi.
5. Mbuzi............. alichinjwa siku ya sikukuu.
6. Mti ............. uliangukia nyumba.

## Zoezi la 4 Utungaji

**Andika shairi lenye beti mbili kuhusu ugonjwa wa Malaria. Shairi lako lizingatie vina na mizani.**

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 134 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Nane

## Haki ya elimu kwa mtoto

Katika sura hii utasoma shairi linalohusu haki ya elimu kwa mtoto. Utaweza kuzijua na kuzielezea haki za watoto katika jamii.

**Fikiri**

1. Haki za mtoto ni zipi?
2. Haki zipi unazipata ukiwa nyumbani?

## Ufahamu

Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali.

### Haki ya elimu kwa mtoto

1. *Vipo vya kupuuzia, si elimu kwa mtoto,*
*Elimu kutupatia, ndio ngao yetu nzito,*
*Viongozi kukazia, sera zilizo mvuto,*
*Elimu izingatiwe, haki ya sisi watoto.*

2. *Haki yetu tupatie, shuleni tupelekeni,*
*Shuleni tujiendee, tusibaki mitaani,*
*Urithi tufurahie, hizo siku za usoni,*
*Elimu izingatiwe, haki ya sisi watoto.*

3. *Haki yetu ni elimu, wazazi zingatieni,*
*Ni suala la muhimu, walezi changamkeni,*
*Bure msingi elimu, walezi tusikieni,*
*Elimu izingatiwe, haki ya sisi watoto.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. *Tupelekeni awali, tusome hadi vidato,*
*Tutakapofika mbali, tutapata na vipato,*
*Tutaepuka ukuli, na ajira za mkato,*
*Elimu izingatiwe, haki ya sisi watoto.*

5. *Yako mengi manufaa, yatokanayo na shule,*
*Ujinga una balaa, tena ni mambo ya kale,*
*Ajira zitatufaa, tuzipe kipaumbele,*
*Elimu izingatiwe, haki ya sisi watoto.*

6. *Maarifa kuyapata, ya kupanua akili,*
*Umasikini kukata, kuondoa kila hali,*
*Maradhi hatutapata, tutajilinda kimwili,*
*Elimu izingatiwe, haki ya sisi watoto.*

7. *Elimu ina ujuzi, maarifa kila fani,*
*Inafaa kwa makuzi, na kwa siku za usoni,*
*Bora kuliko mavazi, hata vitu vya nyumbani,*
*Elimu izingatiwe, haki ya sisi watoto.*

8. *Tamati nimefikia, kalamu namalizia,*
*Watoto kutupatia, elimu ya Tanzania,*
*Hata na Ulaya pia, Mungu akitujalia,*
*Elimu izingatiwe, haki ya sisi watoto.*

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Nani anatakiwa kumpatia mtoto elimu?
2. Shairi hili lina beti ngapi?
3. Ujumbe gani tunaupata katika ubeti wa tatu?
4. Kwa nini wazazi au walezi ni wa muhimu katika kusimamia elimu kwa watoto?
5. Mwandishi ameeleza faida zipi za elimu?



FOR ONLINE USE ONLY

Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 136 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Oanisha maneno ya kifungu A na maana zake katika kifungu B.**

| Kifungu A | Kifungu B |
|---|---|
| i. urithi | (a) inayosaidia kupunguza joto |
| ii. mvuto | (b) janga linalomfika mtu na kusababisha hasara |
| iii. sera | (c) stahili ya mtu |
| iv. maradhi | (d) maarifa ambayo mtu huweza kubobea |
| v. balaa | (e) kuimba shairi |
| vi. kuli | (f) mali au vitu vyote vilivyoachwa na mtu aliyefariki ili vigawiwe |
| vii. fani | (g) kanuni inayoongoza kufikia malengo fulani ya taasisi au nchi |
| viii. tamati | (h) mtu anayebeba mizigo, mchukuzi/mbebaji |
| ix. ghani | (i) mwisho wa mfuatano wa jambo lolote |
| x. haki | (j) kuwa na mwonekano wa kupendeza |
| | (k) mahali pa kuanzia jambo lolote |
| | (l) kinachoathiri afya ya kiumbe, ugonjwa |

## Zoezi la 3 Miundo

**Tunga sentensi kwa kutumia miundo ifuatayo:**

***Mfano:*** *Baraka alisoma kwa bidii <u>hatimaye</u> alifaulu.*

*Alianza na biashara ndogo <u>mwishowe</u> akawa mjasiriamali mkubwa.*

1. ................ hatimaye..............................
2. ................ mwishowe ..........................
3. ................ mpaka ..................................
4. ................ bali ......................................
5. ................ lakini ..................................
6. ................ ingawa ................................

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 137 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

1. Mchelea mwana kulia, _______________
2. ______________________, angali mbichi.
3. Asiyefunzwa na mamaye, _____________
4. Mchagua jembe, ______________________
5. Kuuliza si, ____________________________
6. Kilema si, ______________________________

## Zoezi la 5 Mazoezi ya lugha

**A. Chagua jibu sahihi kujaza nafasi iliyoachwa wazi.**

1. Kituo katika shairi hili ni.........
   (a) Vipo vya kupuuza, si elimu kwa mtoto.
   (b) Elimu izingatiwe, haki ya sisi watoto.
   (c) Shuleni tujiendee, tusibaki mtaani.
   (d) Ni bure hii elimu, wazazi tusikieni.
2. Wajibu wa kutoa elimu kwa watoto ni wa ............
   (a) jamii
   (b) wazee
   (c) wazazi au walezi
   (d) majirani
3. Ubeti wa tatu unaeleza kuwa elimu msingi nchini hutolewa............
   (a) kwa kulipa fedha nyingi
   (b) kwa watu maskini tu
   (c) kwa matajiri tu
   (d) bure



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 138 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Mshairi anaeleza katika ubeti wa saba kuwa elimu ni bora kuliko mavazi……
   (a) Elimu ina ujuzi na maarifa ya msingi maishani.
   (b) Mavazi yanapatikana bila gharama.
   (c) Elimu ni sawa na mavazi.
   (d) Elimu inazingatia umri.
5. Haki ya elimu ya mtoto huanzia elimu ya………..
   (a) kidato cha kwanza
   (b) msingi
   (c) awali
   (d) nyumbani
6. Shairi hili linatufundisha ………..
   (a) kuwabagua watoto
   (b) kuwapenda watoto
   (c) kuwapa ajira watoto
   (d) haki ya elimu kwa watoto

**B. Imba wimbo huu kwa sauti kisha andika haki za mtoto zilizotajwa katika wimbo.**

*Tusipopatiwa upendo, apatiwe nani? x 2*
*Aaa, apatiwe nani x 2*

*Tusipopatiwa elimu, apatiwe nani? x 2*
*Eee, apatiwe nani x 2*

*Tusipopatiwa nafasi, asikilizwe nani? x 2*
*Iii, apatiwe nani x 2*

*Tusipopatiwa mavazi, apatiwe nani? x 2*
*Ooo, apatiwe nani x 2*

*Tusipopatiwa malazi, apatiwe nani? x 2*
*Uuu, apatiwe nani x 2*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 139 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Tunga sentensi kumi (10) kutokana na jedwali lifuatalo:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kijana mwema asiwe | mchonganishi<br>mvivu<br>mwoga<br>mchafu | bali | awe mchapa kazi<br>awe mpole<br>awe mpatanishi<br>awe jasiri |

**D. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika kitendo kwa kila neno ulilopewa.**

***Mfano:*** *wimbo – imba*

1. kilio ___________
2. agizo ___________
3. kipigo ___________
4. kilimo ___________
5. majengo ___________
6. somo ___________

## Zoezi la 6 Vitendawili

**Tegua vitendawili vifuatavyo:**

(a) Nyumba yangu ina mlango juu. ___________

(b) Kilemba chake haazimishi. ___________

(c) Kila niendako ananifuata. ___________

(d) Popoo mbili zavuka mto. ___________

(e) Tajiri wa rangi. ___________

(f) Nyumba yangu ni ndogo lakini ina wapangaji wengi.

___________

## Zoezi la 7 Utungaji

**Tunga shairi lenye beti mbili kuhusu SHULE YETU. Zingatia urari wa vina na mizani.**



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 140 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tisa

## Kufuata maelekezo ya uelekeo wa pande kuu nne za dunia

Katika sura hii utasoma hadithi inayohusu “Safari yetu.” Utajifunza jinsi ya kufuata maelekezo ya uelekeo wa pande kuu nne za dunia na namna ya kuyatekeleza ipasavyo.

**Fikiri**

1. Asubuhi jua linachomoza kutoka upande gani?
2. Jioni jua huzama upande upi?

## Ufahamu

*Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.*

### Safari yetu

Hapo zamani za kale, palikuwa na watoto wanne. Mtoto mkubwa aliitwa Sai, wa pili aliitwa Kulwa, wa tatu aliitwa Nyadu na wa mwisho Mira. Sai alikuwa kifunguamimba wa familia yao na Mira alikuwa kitindamimba. Siku moja watoto hao walipanga safari ya kwenda Kanoti. Walibeba maziwa yaliyojaa kwenye kibuyu, viazi na nyama zilizokaangwa vizuri.

Wakati wanaendelea na maandalizi, walikubaliana kwamba, mdogo wao Mira ndiye atakayebeba vyakula. Ndugu zake hawakujua kuwa Mira alikuwa mchoyo. Alitamani kula vyakula vyote peke yake. Hivyo, akafikiria namna ya **kuwapiga chenga** ndugu zake. Kwa unyenyekevu akawaambia, “Ndugu zangu,

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 141 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

tumebeba vyakula lakini tumesahau maji. Ngoja nikachote." Mira akaondoka na kuelekea mbali upande wa **Kusini**. Akiwa anakwenda, akatazama kulia na kushoto ili kuhakikisha ndugu zake hawamuoni. Alitembea kwa kasi kila **alipopiga hatua** aligeuka nyuma. Alipita katika misitu, vichaka, milima na mabonde. Hatimaye alifika mahali penye kivuli na patulivu. Akasema, "Hapa ndipo nitakapokaa nijifiche na kula chakula chote." Mira alikula chakula chote akashiba na kulala usingizi mzito.

Ndugu zake walimsubiri kwa muda mrefu wasimuone. **Wakakata shauri** kwenda kumtafuta. Walipokuwa wakienda njiani walikutana na bibi kizee. Walifurahi sana wakamsalimia kwa shauku kubwa. Walimuuliza kama amemuona ndugu yao. Bibi aliwajibu kuwa hajamuona. Aliwashauri watawanyike kuelekea pande tofauti, akawaambia, "Mimi nitawasaidia namna ya kumpata ndugu yenu. Nitawaelekeza muelekee pande tofauti. Upande utakapoelekea ndilo litakuwa jina lako siku zote."



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Akamwambia yule mkubwa, "Wewe elekea juu upande wa **Kaskazini**." Sai alifurahi na akamshukuru bibi kisha akaondoka. Alipofika alisema, "Hapa ni juu na pazuri sana. Mira akitokea upande wowote nitamuona."

Bibi alimwambia Kulwa aelekee upande wa kulia wa Sai ambao ni **Mashariki**. Kulwa aliondoka alipofika alisema, "Hapa ndipo nitakapokaa ili nipate kumwona Mira, maana pana mwanga wa kutosha. Upande huu ndiko jua linakochomoza." Bibi alimwambia Nyadu aelekee upande wa kushoto wa Sai ambao ni **Magharibi**. Nyadu alikubali akamshukuru bibi, akaondoka. Alipofika akasema, "Hapa ndipo nitakapomsubiri mdogo wangu, maana ni upande jua linapozama. Bila shaka Mira atakimbilia huku."

Siku zilipita wakimtafuta mdogo wao lakini hawakuweza kumuona. Ndugu hawa huko waliko waliendelea na maisha yao mapya. Mira alijutia kitendo alichowafanyia ndugu zake. Pia aliona aibu kurudi nyumbani. Mira alibadili tabia yake ya uchoyo akawa mtu mwema. Tangu siku hiyo, ndugu hawa hawajaonana tena.

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Taja majina ya watoto wanne waliotajwa katika hadithi hii.
2. Watoto hawa wanne walipanga safari ya kwenda wapi?
3. Waliandaa chakula gani cha safari?
4. Mtoto aliyebeba chakula alikuwa na tabia gani?
5. Watoto wale walimkuta wapi bibi kizee?
6. Unafikiri ni kwa nini wale ndugu hawataonana tena?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi moja kwa kila neno.**

1. Kaskazini
2. Kusini
3. Mashariki
4. Magharibi
5. shaka
6. mchoyo
7. nyenyekea
8. msitu
9. zama
10. chomoza

## Zoezi la 3 Miundo

**Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.**

1. ……………………. **upande wa** ……………………...

***Mfano:*** *Kijiji cha Itiso kiko* ***upande wa*** *Kusini mwa shule yetu.*

(a) ……………………………………........…………

(b) ………………………………......………………….

2. …………………………. **kisha**……….......…………………...

***Mfano:*** *Alielekea Kusini* ***kisha*** *akakaa na kula chakula chote.*

(a) ……………………………………………........…..

(b) …………………………………………….....……..

3. ……….……… **halafu**…….....………………………….....

***Mfano:*** *Tulijiandaa* ***halafu*** *tukaanza safari yetu.*

(a) ………………………………………………………..

(b) ………………………………………………………..

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4 Mazoezi ya lugha

### A. Kanusha sentensi zifuatazo:

1. Jua huzama upande wa Mashariki.
2. Jua huchomoza upande wa Kaskazini.
3. Mira alikutana na ndugu zake.
4. Ili kufika upande wa Mashariki ni lazima kupita upande wa Kusini.
5. Kulwa alikwenda upande wa kushoto wa Sai.

### B. Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali.




Kama madarasa yapo upande wa Kaskazini wa shule. Je,

1. Choo kipo upande gani wa shule?
2. Uwanja wa mpira wa miguu upo upande gani wa shule?



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 145 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Chagua jibu lililo sahihi, kisha andika herufi yake katika kisanduku.**

1. Neno machweo lina maana ya;
   (a) wakati jua linapochomoza
   (b) wakati jua linapokuwa la utosi
   (c) wakati jua linapozama

2. Kinyume cha neno chomoza ni;
   (a) zama
   (b) mwanga
   (c) giza

3. Neno mawio lina maana ya;
   (a) wakati jua linapozama
   (b) wakati jua linapokuwa la utosi
   (c) wakati jua linapochomoza

4. Mtoto wa mwisho kuzaliwa huitwa;
   (a) kifunguamimba
   (b) kitindamimba
   (c) kilindamimba

5. Mtoto wa kwanza kuzaliwa huitwa;
   (a) kifunguamimba
   (b) kitindamimba
   (c) kifungamimba

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 146 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Chagua neno sahihi kutoka katika kisanduku kisha weka kwenye kundi linalostahili.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| sisimizi | chomoza | mbele | bombani |
| tokeza | mavazi | pale | ziwani |
| nanasi | papasi | shati | Kusini |
| pande | karoti | | |

***Mfano:*** *suruali, gauni, sketi, .............*
*suruali, gauni, sketi, shati*

1. kupe, chawa, kunguni, ……………………...
2. Kaskazini, Mashariki, Magharibi, …………...
3. juu, chini, nyuma, …………...
4. mawio, machweo, zama, ……………
5. baharini, mtoni, bwawani, …………
6. embe, papai, chungwa, ………...

**E. Ongeza silabi moja katika maneno yafuatayo ili kuunda neno jipya.**

***Mfano:*** *wanja – uwanja*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. dodo | ……… | 4. ua | …………. |
| 2. bao | ……... | 5. gomba | ………… |
| 3. lia | ……… | 6. moja | ………… |

**F. Andika wingi wa maneno haya.**

| | Umoja | Wingi | | Umoja | Wingi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | mkoa | ________ | 4. | upande | ________ |
| 2. | uwanja | ________ | 5. | kitunguu | ________ |
| 3. | choo | ________ | | | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**G. Kamilisha fumbo hili kwa kujaza nafasi kwa kwenda chini na kwenda kulia.**

**Kwenda chini**

1. Kifaa kinachoonesha pande kuu za dunia (4)
2. Nyota inayotawala wakati wa mchana ambayo huchomoza Mashariki wakati wa asubuhi na kuzama Magharibi wakati wa jioni. (3)
3. Kipindi cha asubuhi wakati wa kuchomoza jua. (5)

**Kwenda kulia**

3. Upande ambako jua huchomoza. (9)
4. Muda wa kuzama jua. (6)
5. Mwinuko mdogo wa ardhi katika eneo tambarare. (6)
6. Upande ambako jua huzama. (9)




**Zoezi la 5 Kazi ya kufanya**

**Toka ndani ya darasa lako. Andika vitu unavyoviona upande wa mbele, kushoto, kulia na nyuma.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Ishirini

## Kusoma ngonjera kwa sauti

Katika sura hii utasoma ngonjera inayohusu wajibu wa mtoto katika familia. Utajifunza namna ya kusoma ngonjera kwa sauti ya kutamba. Utaweza kuandika habari fupi kuhusu wajibu wa mtoto katika familia yake. Vilevile utaweza kueleza umuhimu wa viungo vya mwili.

**Fikiri**

Mambo gani unayopaswa kufanya kama wajibu wako?

FOR ONLINE USE ONLY

## Ufahamu

Soma ngonjera ifuatayo, kisha jibu maswali.

### Wajibu wa mtoto katika familia

**Neema:**

*Leo ni siku murua,*
*Habari nawaletea,*
*Taarifa kuitoa,*
*Ya wajibu wa watoto.*

**Musa:**

*Wengi wetu twaujua,*
*Huna haja kutwambia,*
*Lipi tusilolijua,*
*Juu ya wajibu wetu.*



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 149 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Neema:** *Subiri uhabarike,*
*Uelewe mana yake,*
*wajibu ueleweke,*
*Daima tuzingatie.*

**Musa:** *Kwani ni lazima sana,*
*Kila jambo kupeana,*
*Wajibu kuambiana,*
*Kuna umuhimu gani?*

**Neema:** *Kila tutakapopita,*
*Shughuli nyingi twapata,*
*Majukumu ya utata,*
*Si halali kwetu hata!*

**Asha:** *Wajibu wetu watoto,*
*Sio kuzoa kokoto,*
*Tusipewe kazi nzito,*
*Kwa kipindi cha mpito.*

**Neema:** *Tujioshee na vyombo,*
*Huku tukiimba nyimbo,*
*Na kufanya kila jambo,*
*Kazi pasipo mgomo.*

**Musa:** *Si lazima kuzitenda,*
*Shughuli tusizopenda,*
*Michezo tunaipenda,*
*Kutwa tunajichezea.*

**Asha:** *Mama zetu saidia,*
*Kufua na kufagia,*
*Kazi hizi twazijua,*
*Ni wajibu wetu pia.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Musa:** *Yote hayo ni ya nini,*
*Sisi watoto jamani,*
*Tutafanya ukubwani,*
*Wakati utapofika.*

**Mwalimu:** *Watoto msipotoke,*
*Kitako msibweteke,*
*Kila moja kazi zake,*
*Kwa hiari azifanye.*

**Mwalimu:** *Na wote walozoea,*
*Watoto kuwaonea,*
*Sio jambo la sawia,*
*Mateso kuwafanyia.*

**Neema na Asha:** *Twapenda kuwausia,*
*Watoto wa Tanzania,*
*Wa Ulaya na Asia,*
*Kutenda wajibu wetu.*

**Wote:** *Sasa tumeshaamua,*
*Wajibu kuzingatia,*
*Sote tutafwatilia,*
*Kazi tutajifanyia.*

## Zoezi la 1 Ufahamu

1. Katika ngonjera hii ni nani anapingana na hoja ya watoto kutimiza wajibu wao?
2. Nani anawashauri watoto kutobweteka?
3. Ngonjera hii inatufundisha nini?
4. Nani anaonekana kutopenda kuwajibika?
5. Musa anapenda kufanya shughuli gani?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 151 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2 Msamiati

**Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

1. zoa
2. bweteka
3. kitako
4. potoka
5. mgomo
6. mpito

## Zoezi la 3 Nahau

**Oanisha sehemu A na B kwa kuandika jibu sahihi.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| i. unga mkono | (a) pata taabu |
| ii. kuwa macho | (b) fariki |
| iii. piga chenga | (c) pata nafuu |
| iv. tia chumvi | (d) sema maneno ya mwisho kabla ya kufariki au kuondoka |
| v. vunja moyo | (e) katisha tamaa |
| vi. toa wosia | (f) kwepa |
| vii. pata ahueni | (g) fika mwisho |
| viii. kata roho | (h) kuwa mwangalifu |
| ix. ona cha mtemakuni | (i) kubaliana |
| x. tia nanga | (j) ongeza maneno yasiyo ya kweli |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4 Miundo

**Tunga sentensi mbili kwa kila muundo ufuatao:**

**1.** …………. sita____ ……………

***Mfano:*** *Ninajutia kupoteza muda kwa kuwa **sita**weza kumaliza kazi.*

(a) …………………………………

(b) …………………………………

**2.** ………………. ili ……………

***Mfano:*** *Baada ya kumlisha mtoto nilimuogesha **ili** alale.*

(a) ……………………………

(b) ……………………………

**3.** ……………. akawa……………

***Mfano:*** *Alizingatia kusoma kwa bidii **akawa** wa kwanza.*

(a) ……………………………………

(b) ……………………………………..

## Zoezi la 5 Methali

**Kamilisha methali zifuatazo:**

**1.** ____________, ila kwa ncha ya upanga.

**2.** ____________, humaliza buyu la asali.

**3.** Mla nawe hafi nawe ila, ___________.

**4.** Mgaagaa na upwa, ____________.

**5.** ____________, halimpati mwewe.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6 Mazoezi ya lugha

**A. Chagua jibu lililo sahihi, kisha andika herufi yake katika kisanduku.**

1. Kazi nzito alizoshauri Asha wasipewe watoto ni kama;
   (a) Kuosha vyombo.
   (b) Kuzoa kokoto.
   (c) Kufagia nyumba.
   (d) Kucheza mpira.

2. Ngonjera uliyotamba inahamasisha;
   (a) Watoto kutimiza wajibu wao.
   (b) Watu wazima kufanya kazi kwa bidii.
   (c) Watoto wapumzike.
   (d) Watoto wafurahi.

3. Mwalimu alitoa ushauri gani kwa watoto?
   (a) Kila mmoja acheze tu.
   (b) Kufanya kazi kwa hiari.
   (c) Kuwapenda watoto.
   (d) Kila mmoja aongee sana.

4. ........………....…ni wajibu wa watoto pia.
   (a) Kufua na kufagia
   (b) Kucheza na kulala
   (c) Kuimba nyimbo
   (d) Kutoa taarifa kwa wengine

5. Kufanya kazi kwa hiari ina maana sawa na;
   (a) Kufanya kazi kwa lazima.
   (b) Kufanya mgomo.
   (c) Kufanya kazi bila kulazimishwa.
   (d) Kufanya kazi huku unaimba.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 154 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B.** **Chunguza picha zifuatazo kisha bainisha kazi ambazo zinamfaa mtoto. Andika sababu kwa nini kazi hizo zinamfaa.**

**1.**



**2.**



**3.**



**4.**



**5.**





Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 155 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Andika neno lenye maana sawa na neno lililopigiwa mstari.**

***Mfano:* <u>Nyanya</u>** *yetu ana mapengo hawezi kula nyama.*

**<u>*Bibi*</u>** *yetu ana mapengo hawezi kula nyama.*

1. Nyumba nyingi zili<u>bomolewa</u> na mafuriko.
2. Mwalimu wetu ni <u>bingwa</u> wa kufundisha somo la Kiswahili.
3. <u>Mbogo</u> ni mkali kuliko ng'ombe.
4. Shangazi alini<u>subiri</u> tusafiri pamoja.
5. Watalii wali<u>kwea</u> mlima Kilimanjaro.
6. Sisi tuna<u>mwagilia</u> bustani yetu ya mboga asubuhi.
7. Walimu wote wana<u>hifadhi</u> vitabu vyao kabatini.
8. Busia ali<u>kiri</u> kuwa ndiye aliyeiba kuku wa jirani.

**D. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

1. nzito ___________
2. penda ___________
3. chache ___________
4. baridi ___________
5. zubaa ___________
6. shusha ___________

**E. Andika umoja au wingi wa maneno yafuatayo:**

| | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| 1. | mwili | ___________ |
| 2. | ___________ | uji |
| 3. | chombo | ___________ |
| 4. | kazi | ___________ |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 156 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. __________ watumwa
6. ungo __________
7. __________ minazi
8. dagaa __________

## Zoezi la 7 Utungaji

**Chunguza picha zifuatazo kisha malizia habari kuhusu wajibu wa mtoto katika familia.**

Watoto ni sehemu ya familia. Wanapaswa kufanya kazi mbalimbali wanazoweza kuzifanya. Pia wanapaswa kujisomea wanapokuwa nyumbani. Mimi na ndugu zangu tunawasaidia kazi wazazi na walezi wetu. Kaka yangu anapoamka ........................

1.





Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 157 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2.



3.



FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 158 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4.



5.



6.






Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 159 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ufahamu

**Soma majigambo yafuatayo kisha jibu maswali.**

**Macho:**
*Mimi ndiyo macho,*
*Huwezi ona bila mimi,*
*Utajikwaa kila mahali,*
*Vidonda mwili mzima,*
*Nani kama macho?*

**Pua:**
*Macho wanichekesha,*
*Tena waniacha hoi,*
*Pua bila kunusa,*
*Maisha yako hatarini,*
*Nani kama pua?*

**Sikio:**
*Mimi kiboko yenu,*
*Giza halinisumbui,*
*Mawimbi tu yatosha,*
*Kusikia hatari zote,*
*Nani kama sikio?*

**Mdomo:**
*Mimi funga kazi,*
*Wote mwanitegemea,*
*Chakula kuwapatia,*
*Kazi zenu kuzitimiza,*
*Nani kama mdomo?*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 160 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kichwa:** *Kichwa ndiyo msingi,*
*Ninyi nyote nawabeba,*
*Kazi zenu hazifanyiki,*
*Bila mimi kuhusika,*
*Ni nani kama kichwa?*

**Kifua:** *Nyote ninyi shikizi,*
*Mimi ndio kila kitu,*
*Moyo umo ndani mwangu,*
*Nikitoka mwapotea,*
*Nani kama kifua?*

**Shingo:** *Hebu acheni kelele,*
*Sisi sote ni ndugu,*
*Macho, pua na sikio,*
*Mdomo na kichwa sikia,*
*Sote twategemeana,*
*Ni vema tushirikiane.*

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 161 7/23/21 3:00 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 8 Ufahamu

1. Taja kazi nyingine za mdomo?
2. Nani anaweza kufanya kazi zake mwenyewe?
3. Unafikiri mshindi ni nani kati ya pua,macho, sikio, mdomo, kichwa, shingo na kifua?
4. Wewe ungependa kuwa nani?
5. Unawashauri nini pua,macho, sikio, mdomo,kichwa, shingo na kifua?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahil STD 4 MARCH 15 2018.indd 162 7/23/21 3:00 PM

## Vitabu vingine kutoka
## Taasisi ya Elimu Tanzania

### Darasa la Nne



















ISBN 978-9976-61-725-2

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne